Kikao cha Nne - Tarehe 15 Oktoba, 2013

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti, (Mahmoud Muhammed Mussa) Alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kuweka mezani Mswada wa Sheria ya Kufuta na Kuandikwa Upya Sheria inayohusu Kampuni na Jumuiya Nyengine, Kuweka Masharti Madhubuti Zaidi ya Uratibu na Udhibiti wa Kampuni, Jumuiya na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Ussi Jecha Simai (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha hati mezani juu ya maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta na Kuandikwa Upya Sheria inayohusu Kampuni na Jumuiya Nyengine, Kuweka Masharti Madhubuti Zaidi ya Uratibu na Udhibiti wa Kampuni, Jumuiya na Mambo Yanayohusiana na Hayo. Naomba kuwasilisha.

MASWALI
Nam. 1
Ukarabati wa Maegesho ya Magari ya Chake Chake

Mhe. Salim Abdalla Hamad (Kny: Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza**:**
Baraza la Mji wa Chake Chake mara nyingi limekuwa makini katika kukusanya kodi sio tu kwenye maduka na wafanyabiashara wadogo wadogo lakini limekuwa madhubuti sana katika kukusanya kodi za maegesho ya magari, magari ya

Ng'ombe na hata Punda na Boda boda, jambo ambalo limesaidia sana katika kuingiza mapato yake.

Kwa kuwa kodi za wananchi zinatakiwa ziwarejee wenyewe kwa kuwapatia huduma mbali mbali jambo ambalo Baraza hilo limekuwa likisuasua kulifanya, Je, ni lini Baraza hilo litafanya ukarabati wa Maegesho ya magari pamoja na barabara ikiwemo ile inayotoka Mahakamani kupitia Hospitali ya Chake kwenda soko la samaki (Qatar) hadi Uwanja wa mpira Tibirinzi?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ – Alijibu**:**

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 1 na kabla ya kujibu naomba kutoa maelezo yafuatayo.

Ujenzi wa maegesho ya magari katika maeneo ya miji ni jukumu la utawala la mji husika, kazi ambayo wanaweza kuifanya wenyewe au kutumia wakala aliyeteuliwa na uongozi wa mji huo.

Aidha, mamlaka za miji pia zina jukumu la kuzisimamia barabara ndogo ndani ya miji husika. Baraza la Mji wa Chake Chake linao mpango wa kuimarisha huduma za maegesho na kuzikarabati barabara za ndani kwa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Changamoto kubwa ambayo mji wa Chake Chake inakabiliwa nayo ni uchache wa nafasi na hali ya milima katika eneo la mji huo kunakopelekea kutokuwa na eneo la kutosha la kujenga maegesho ya magari yanayoingia katika mji huo ambao ni kituo kikubwa cha kibiashara na Makao Makuu ya afisi nyingi kwa upande wa Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo.

Baraza la Mji wa Chake Chake linategemea kujenga maegesho ya magari katika maeneo ambayo yana nafasi na maeneo yanayoendelezwa likiwemo soko la Qatar. Aidha Baraza la Mji la Chake Chake limeshawasiliana na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa ajili ya ukarabati wa barabara itokayo hospitali ya Chake Chake hadi njia ya kwenda uwanja wa Kibirizi.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kwanza ninashukuru kwa kupata majibu mazuri na mimi nina swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, katika majibu yake Mhe. Waziri amesema kuwa Baraza la Mji tayari limeshawasiliana na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kuifanyia ukarabati barabara inayotoka Makamakani moja kwa moja mpaka Qatar. Lakini kwa sababu barabara hii ni mbaya sana na inatumika siku zote na hasa hivi sasa kwa sababu ya lile soko la Qatar, na kwa sababu hili Baraza la Mji halijaanza leo siku zote lipo, na lipo Chake Chake na linaiona ile hali.

Mawasiliano haya ni kuwa utekelezaji wake utakuwa lini hasa kutokana na shida iliopo ya usafiri. Hilo ni moja.
Halafu la pili, tulipata taarifa hapa kuwa serikali kwa makusudi ilitaja sehemu kule Chake Chake ambapo itajenga maegesho haya ya magari...

Mhe. Mwenyekiti: Samahani Mhe. Mjumbe, Mhe. Waziri hakusikii vizuri huku. Kwa hivyo itabidi urudi tena na hiyo *speaker* itabidi uisogelee.Rudia swali na sio maelezo.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, maswali yangu ni lazima yawe na maelezo.

Swali ni hivi kwa sababu Mhe. Waziri amesema kuwa Baraza la Mji limewasiliana na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kuifanyia ukarabati hii barabara iliyotajwa, lakini kwa sababu barabara hii ni mbovu tokea zamani sana na inatumika sana kweli kweli na hasa kwa sababu ya kuwepo lile soko la Qatar. Jee, ni lini hasa itajengwa baada ya mawasiliano hayo kwa sababu hakutaja hasa siku rasmi ambayo itaanza kujengwa. Hilo ni swali la mwanzo.

Swali la pili. Lilikuja suala hili la kutafuta sehemu ya maegesho ya magari katika mji wa Chake Chake kutokana na nafasi finyu iliopo ambayo pia imo katika hali mbaya sana, na tukaambiwa ipo sehemu ambayo itafanyiwa marekebisho na kuwekwa sehemu hii ya kuegesha magari. Lakini leo kwa sababu Mhe. Waziri kasema kuwa Chake Chake kuna milima na yale ni mambo ya Mwenyezi Mungu hayawezi kuepukika, ina maana ndio maana milima hasa ni sababu ya kutokuwa na maegesho ya kuegesha magari yetu mpaka leo iwe tunakwenda mpaka leo katika msongamano ule tulionao.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake ya nyongeza kama ifuatavyo.

Ni lini barabara itajengwa kutokana na uchakavu wake hasa kwa sababu barabara ile hivi sasa inatumika sana?
Nataka nikubaliane naye kwamba barabara ile sasa kutokana na kupelekwa kwa soko la samaki pale inatumika kweli kweli na tokea zamani inatumika, kwa sababu itakumbukwa kwamba tokea zamani hata kama kabla ya lile soko halijahamishiwa pale, barabara ile inatumika kama inavyotumika sasa. Kwa sababu magari yote yaliyokwenda katika *stand* ya zamani au *stand* iliopo kwenye mji wa Chake Chake ni lazima yazungukie huku njia ya Tibirinzi na mengine yanazungumzia ile njia ya kutokezea Miembeni.

Lakini lini itajengwa barabara? Itajengwa pale ambapo hali ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Barabara zitakapofikishwa kwenye Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ili ziweze kutumika kwa ajili ya kazi hiyo.

Swali lake la pili. Nilipokuwa nikijibu swali nilisema kuwa mji wa Chake Chake una milima, na milima ni kazi ya Mwenyezi Mungu, na mimi nataka nikubaliane naye kutokana na hiyo kazi ya Mwenyezi Mungu ndio sisi Baraza la Mji Chake Chake tunawajibika kutafakari na kuangalia baada ya mipango miji kuweza kutafuta eneo muafaka la kuweza kujenga maegesho ya magari hasa kutokana na mji wa Chake Chake hivi sasa katika maeneo mengi yameshaanza kujengwa majengo mengi sana katika maeneo yale.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, kunipatia nafasi ili niweze kumuuliza Mhe. Waziri swali moja lenye sehemu mbili la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Waziri kwanza nikupongeze kwa kuteuliwa katika wizara hii, ni imani yangu kwamba utafanya kazi vizuri na utavaa vizuri viatu alivyoviacha Dr. Mwinyihaji.

Mhe. Waziri Baraza la Mji wa Chake Chake lilikuwa na mpango wa kujenga *stand* mpya ya kisasa katika bonde la Mava Mbarouk.

Naomba nikuulize Mhe. Waziri ni mara ngapi umelitembelea bonde hilo ili na wewe kuangalia uwezekano wa kufanya kazi hiyo.

Swali la pili. Kama hivyo ndivyo basi ni lini serikali kupitia Baraza la Mji litaijenga rasmi ***stand*** hiyo?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi.
Baraza la Mji wa Chake Chake kweli lilitenga eneo ambalo amelitaja Mhe. Mwakilishi kujenga *stand* ya magari badala ya *stand* iliopo hivi sasa, ni lini limetembelea eneo hili?

Tokea nimeteuliwa ni mwezi mmoja na nusu. Nimeshafanya ziara ya kwenda kutembelea mji wa Chake Chake lakini sijabahatika kwenda kutembelea eneo hili, lakini baada ya kwisha kukamilisha ziara yangu ninayoifanya sasa katika Idara Maalum, nategemea kwenda Pemba kwa ajili ya kumalizia ziara yangu kwenye Idara, katika wakati huo nitajipa muda wa kwenda kulitembelea eneo ambalo linatarajiwa kujengwa *stand* ya magari katika mji wa Chake Chake.

Swali lake pili, serikali au Baraza la Mji wa Chake Chake ni lini inatarajia kuijenga *stand* hiyo? Baada ya kukamilisha mipango na michoro itakayokuwa imekusudiwa kwa ajili ya ujenzi wa *stand* ya magari. Baraza la Mji kwa kutumia fedha zake au kwa kutafuta mwekezaji ambaye atakuwa ana uwezo wa kufanya kazi hiyo kwa makubaliano maalumu na Baraza la Mji, tutaijenga *stand* hiyo.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Mwenyekiti, na mimi vile vile nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na pia niungane na wenzangu katika kumpongeza Mhe. Waziri kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye vifungu vitatu.
Mhe. Waziri kuna mradi unaoitwa Mradi wa Huduma za Miji *(Zanzibar Urban Service Program).* Jee, mradi huu unafadhiliwa na nani na ni wa kiasi gani, ni msaada au mkopo?

Lakini ni mambo gani makubwa na utagharimu kiasi gani katika mradi huu kwa ajili ya mji wa Chake Chake tu?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Kweli upo mradi wa *ZUSP* ambao unafadhiliwa na World Bank katika miji yetu ya Baraza la Mji wa Unguja, Baraza la Mji Chake Chake, Baraza la Mji Wete na Baraza la Mji Mkoani.
Ni kiasi gani ambacho kinafadhiliwa kwenye mradi huu. Ni karibu dola milioni 38. Katika dola hizo milioni thalathini na nane kwa sasa hivi siwezi kusema ni ngapi Baraza la Mji la Zanzibar na Mabaraza ya Miji, lakini ninaahidi kumletea *break down* ya kila Baraza la Mji fedha ambazo wanawasilishiwa kwa maandishi Mhe. Mwenyekiti. Ahsante sana.

Nam. 95
Biashara ya Nguo za Ndani za Wanawake

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza**:**

Tanzania Bara imepiga marufuku uingizaji wa nguo za ndani za wanawake kwa sababu za kiafya, lakini nguo hizo bado zinaingizwa na kuuzwa hapa Zanzibar bila ya kuzingatia usalama kwa wananchi wanaotumia nguo hizo.

(a) Serikali ina mpango gani wa kuzuia nguo hizo kwa usalama wa wananchi wake.

(b) Katika kulinda heshima ya nchi, kwa nini nguo aina hiyo zisipigwe marufuku na badala yake ziruhusiwe nguo za mitumba za kawaida?

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko – Alijibu**:-**

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 95 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ina jukumu kubwa la kuwalinda wananchi wake kutokana na madhara ya bidhaa zozote zinazokuja kibiashara. Pia ina wajibu wa kupiga marufuku uuzwaji na usambazaji wa bidhaa yoyote ambayo itathibitika kiafya ina madhara kwa binadamu.

Kuhusu mitumba ya nguo za ndani, Wizara haijapokea malalamiko yoyote kuhusu nguo hizo kutoka kwa watumiaji na wala hakuna ushahidi wa kitaalamu kuwa nguo hizo ambazo zinaletwa katika soko la Zanzibar zina madhara kwa matumizi ya binadamu. Hata hivyo, kwa vile suala hili sasa linaonekana kufanyika kwa kasi, Wizara ya Biashara kupitia Kitengo cha Kusimamia na Kumlinda Mtumiaji ikishirikiana na Taasisi ya Viwango ya Zanzibar na Wizara ya Afya italifuatilia suala hili ikiwa ni pamoja na kufanya uchunguzi wa kina kupata ushauri wa kiafya.

Mhe. Mwenyekiti, endapo itathibitika basi kwamba nguo hizi zina madhara, wizara kupitia SMZ haitosita kuchukua hatua muafaka ikiwa ni pamoja na kuzipiga marufuku nguo hizi pale itakapobidi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri jirani yangu hapa na vile vile siwezi kufika Jimbo la Muyuni bila ya kupita katika Jimbo la Fuoni, naomba kuuliza maswali mawili madogo tu ya nyongeza.

Serikali ya Muungano jana imetangaza rasmi kuhusu uingizwaji wa nguo za ndani za wanawake (mitumba) kutokana na sababu za kiafya kwa kuwa usalama wao umekuwa ni mdogo. Vile vile

serikali ya Malawi mwaka huu mwezi wa Septemba imetangaza rasmi kuangalia sheria hiyo.

Jee, huoni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuendelea kuruhusu uuzwaji wa nguo hizo?
Swali la pili kwa kuwa hoja ni ya kulinda afya za wananchi, kuendelea na nguo hizo kuuzwa Zanzibar kutaleta sura gani na ukiangalia wananchi wa Zanzibar ni sawa wa Tanzania Bara na wale wa Malawi?

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, nimesema katika jibu la swali la msingi kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia wizara itafanya uchunguzi kwa sababu sasa imepokea suala hili na tutalifanyia kazi kwa pamoja. Kitengo chetu cha Kumlinda Mtumiaji lakini na Wizara ya Afya tutashirikiana, na endapo ikithibitika kwamba nguo hizi zina madhara basi serikali kupitia wizara hii haitosita kuzipiga marufuku hizi nguo kama zitakuwa zina madhara.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kuweza kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Naibu Waziri.

Kwanza nimshukuru sana kwa kauli yake hiyo aliyosema hapa, kwanza utakubaliana na mimi kuwa tayari hizo nguo sasa hivi zimeshaleta madhara kwa akina mama.
Lakini swali la pili, Mhe. Naibu Waziri kuwa serikali isubiri mpaka litokezee tatizo, huoni kuwa tutawadhoofisha wananchi wetu kutokana na uchunguzi wetu wa serikali kutokamilika mapema.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.
Anasema hapa Mheshimiwa kwamba tayari nguo hizi zimeshaanza kuonesha madhara. Basi tutamuomba ashirikiane na wizara ili tuweze kulifanyia kazi suala hilo. (*Makofi*).
Lakini nikubaliane naye Mhe. Mwakilishi kwamba hakuna haja ya kusubiri mpaka madhara yatokee. Ndio maana tukasema kwamba hivi sasa tunalifanyia kazi suala hili kwa kuwa limeshajitokeza, na kwa hivyo tutaomba sana mashirikiano yake katika kulifanyia kazi hilo.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza.
Mhe. Naibu Waziri licha ya nguo hizi kuwa na madhara kwa akinamama lakini pia nguo hizi ni mastuhu kwa akinamama, nikiwemo mimi na wewe. Jee, Mhe. Naibu Waziri ikiwa nguo hizi ni mastuhu na ikiwemo mimi na wewe; mastuhu ninadhani maana yake hujafahamu.

Mhe. Mwenyekiti: Bado hatujafahamu hata mimi pia huku.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Maana yake ni kitu cha siri tuseme, maana yake kama kitu cha staha.

Mhe. Naibu Waziri naomba nirudie kwa kuwa licha ya nguo hizi kuwa na madhara lakini pia nguo hizi ni mastuhu kwa akinamama nikiwemo mimi pamoja na wewe na wanaume wengine. Jee, Mhe. Naibu Waziri huoni kuwa suala hili kulipiga vita ni kitu muafaka kwa hivi sasa? Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi ...

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe ingelikuwa jambo la busara tukamsikiliza Mhe. Naibu Waziri anapotoa jawabu ili yule aliyeuliza swali aweze kufahamu vizuri zaidi.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubaliana naye moja kwa moja na katika kulifanyia kazi suala hili, sio tu tupate mashirikiano na Mhe. Makame Mshimba au Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mheshimiwa yeyote ndani ya Baraza hili tutahitaji mashirikiano yake kwenye kulifanyia kazi suala hili ili kama zina madhara basi tuone kwamba wananchi wetu hawapati madhara yanayotokana na nguo hizi.

Na. 15
Kushajihisha Wakulima Katika Kilimo cha Maua

Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Aliuliza**:-**
Kilimo cha maua (*floriculture*) katika nchi za wenzetu kimekuwa na tija sana ambapo kimesaidia wakulima wa kilimo hicho kupunguza umasikini na kuongeza kipato.

(a) Je, ni lini Serikali itawashajihisha wakulima wa hapa visiwani Zanzibar kulima kilimo cha maua ili nao wafaidike na faida ya kilimo hicho kama ilivyo kwa wenzetu.

(b) Kwa hapa Zanzibar ni maeneo gani ambayo kilimo cha maua (*floriculture*) kinanawiri vizuri.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili.- Alijibu**:-**
Mhe. Mwenyekiti**,** kabla sijamjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake lenye vifungu (a), (b), kwanza naomba kutoa maelezo mafupi kuhusiana na kilimo cha maua kama ifuatavyo:-
a)Suala la aina gani ya kilimo mkulima alime ni uamuzi wa mkulima mwenyewe, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo wajibu

wake ni kutoa utaalamu kwa mkulima yeyote atakayetaka kulima mazao ya chakula au ya biashara kama maua.

Aidha, Wizara ya Kilimo inatoa maelekezo kwa wakulima juu ya namna ya kujitayarisha kwa kilimo chochote anachotaka na jinsi ya upatikanaji wa nyenzo na masoko.

Mhe. Mwenyekiti**,** uanzishwaji wa kilimo cha maua unahitaji mtaji mkubwa ikiwemo ujenzi wa miundombinu iliyo imara na gharama nyengine za pembejeo na vibarua. Pia kilimo cha maua kinahitaji eneo la ardhi la kutosha na mahitaji makubwa ya vibarua na udhibiti wa maradhi na wadudu. Hivyo hayo yote ni gharama kubwa zinazohitaji mwekezaji kujipanga vizuri, lakini kwa mwananchi yeyote anayetaka kulima kilimo hicho milango iko wazi na afike wizarani kwa maelekezo.

b)Mhe. Mwenyekiti, kilimo cha maua hapa Zanzibar kinaweza kunawiri popote mradi miundombinu inayohitajika ijengwe, kwa sababu kilimo hiki cha maua hakilimwi katika maeneo ya wazi. Majengo maalum yanahitajika kwa maua ili kuyahifadhi katika mazingira maalum ya kuweza kumea vizuri. Hali ya hewa katika maeneo ya wazi inaharibu kilimo chote cha maua, hasa kwa nchi za joto kama Zanzibar.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mhe.Naibu Waziri kwa sababu katika jibu lake amesema kwamba kilimo hicho kinahitaji mtaji mkubwa sana. Nilikuwa nataka kujua ni kiasi gani cha mtaji ambacho kinachohitajika.

Lakini swali la pili, nimuulize Mhe. Naibu Waziri kwa hivi sasa Zanzibar yupo mwekezaji ambaye anashajihisha kilimo cha *green tea* ambacho kilimo cha maua kinanawiri sana katika

teknojia ile. Jee, serikali haioni kwamba umefika wakati kushirikiana na mwekezaji yule ili kuona kwamba wananchi wanakuwa na kilimo mbadala baada ya kile cha mboga mboga tu. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo.
Mhe. Mwenyekiti, tukichukulia suala la majengo kwamba tupate *screen house*. *Screen house* moja inachukua milioni nane. Kwa hivyo bado huo ni mzigo, ni gharama kwa kilimo hiki mbali mahitaji mengine.

Swali la pili la kushirikiana na mwekezaji, serikali kama nilivyosema kwamba kilimo hiki ni gharama, huyo mwekezaji ambaye aliyekuwepo anashughulikia kilimo hiki kweli na yeye alijipanga vya kutosha ndipo akaweza kuhimili kilimo hiki.
Bado tunasema mtu yeyote anayetaka kulima kilimo, kwa hivyo sisi tutatoa taaluma aje tumpe taaluma ili akaanzishe kilimo hicho.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuuliza swali hili kidogo ningetoa neno moja naomba kwa ruhusa yako.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba mimi serikali ikanihurumia na mimi ikanipa Waziri wa kilimo ili kuweza kumsaidia Mheshimiwa wangu Mhe. Naibu Waziri kwa sababu anaweza kufika pahala akaja akashindwa. (*Makofi*).

Sasa ninakuja kuuliza swali la nyongeza.
Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, kuna vijana wamejitokeza kwa makusudi wapo Tunguu wanalima mambo haya ya maua maua.

a) Je, wizara yako Mhe. Waziri inawasaidia nini wale vijana ili na wao waondokane na umaskini.

b) Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni nilimsikia Mhe. Waziri alisema kuwa maeneo mengi yaliyochukuliwa kule sehemu ya Selemu yatafutwa na wewe ulisema katika jibu lako mama kuwa hakuna pungufu ya maeneo. Je, lile suala limeshafutwa na wananchi wameshaanza kupewa ili waweze kuelimishwa kuweza kupanda maua.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, kweli Tunguu kuna wakulima ambao wanalima maua, lakini wakulima hawa tunachowasaidia ni kuwapa taaluma, kwa sababu wizara yangu kazi yake ni kutoa taaluma kwa mkulima yeyote. Kwa hivyo, wakulima hawa wanapohitaji wanafika wizarani na kupatiwa taaluma.

Jibu jengine ni kwamba maeneo ya Selemu bado hayajagaiwa kama nilivyosema, lakini bado tunasema tuna upungufu wa maeneo ya kulima kilimo cha maua, hasa kilimo hiki kinavyohitajika kwenye maeneo maalum.

Nam. 11

Juhudi za Kuwawezesha Wavuvi Wadogo Wadogo

Mhe. Hassan Hamad Omar (Jimbo la Kojani)Aliuliza:-

Serikali imeonesha juhudi na dhamira njema kwa wananchi wake kwa kuweka mikakati ya kukuza uchumi na kupunguza umasikini. Suala hilo Wizara ya Mifugo na Uvuvi ililipokea vyema na kuahidi kuwaboresha wavuvi wadogo wadogo na kuandaa mipango mizuri ya kufikia Uvuvi wa bahari kuu.

(a) Je, ni juhudi gani zilizochukuliwa na Wizara katika kuwawezesha wavuvi wadogo wadogo ili waweze kuendelea kibiashara zaidi.

(b) Je, wizara yako imefikia hatua gani katika kuelekea uvuvi wa bahari kuu.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Alijibu:-

Mheshimiwa Spika naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi suali lake namba 11 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika,

a) Wizara yangu ili kuwafanya wavuvi wetu kuenda kibiashara, imefanya juhudi mbali mbali ikiwa ni pamoja na kujenga masoko katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba na kuyatia majokofu kwa ajili ya kuhifadhia samaki wakati wavuvi wamechelewa kurudi baharini au wamekosa wanunuzi wanaporejea kuvua ili waweze kuuza bidhaa zao wakati mwengine na kupata bei ya tija zaidi. Aidha Wizara yangu kupitia Mradi wa **MACEMP** ilitoa vyombo na vifaa vya kufanyia kazi kwa vikundi mbali mbali vya uvuvi kama boti za uvuvi, nyavu na mashine. Hatua hii ilianza katika mwaka 2005 kwa lengo la kuwawezesha wavuvi kwenda kuvua masafa ya mbali zaidi na kupata mapato zaidi.

b) Kuhusu suala la Bahari Kuu, Wizara yangu inaendelea na utaratibu wa kuvipata vyombo vya kisasa vya uvuvi kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa vijana na kujenga uwezo wa watakaopewa mafunzo hayo ili waweze kuua aina ya uvuvi watakaoshughulika nao na kuendesha vyombo hivyo

kwa kufuata sheria za Kimataifa. Hii itatoa uzoefu wa kufanya kazi katika maji ya kina kirefu ambapo itapelekea wavuvi hao kuwa baharini kwa zaidi ya masaa 24 mpaka wiki moja, badala ya mazoea ya kwenda na kurudi kwa masaa machache kwa hivi sasa.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Kwa sababu Mhe. Naibu Waziri umesema katika mradi wa MACEMP umesaidia sehemu mbali mbali, kutoa vyombo kama mashine na kujenga majokofu ya kuhifadhia samaki.

a) Mhe. Mwenyekiti, naomba kujua ni sehemu gani vilipotiwa vifaa hivyo na hayo majokofu yamejengwa wapi?

Mhe. Mwenyekiti: Samahani, hebu sogelea hicho kipaza sauti kidogo ili tuweze kukusikia vizuri. Mhe. Naibu Waziri hilo swali (a) umelisikia au vipi.

Mhe. Hassan Hamad Omar: (a) Mhe. Mwenyekiti, swali langu la nyongeza ni kwamba kwa sababu umesema kwa kupitia mradi wa MACEMP umesaidia zana mbali mbali za kiuvuvi, ikiwemo mashine. Nataka kujua ni sehemu ngapi umesaidia na hayo majokofu yaliyojengwa kwa kuhifadhia samaki ni wapi yamejengwa?

b) Kwa sababu wizara yako imekusudia kwenda kwenye uvuvi wa bahari kuu na umesema iko katika mipango ya kuelekea huko. Ninavyofahamu mimi kama ni meli ya wavuvi inachuku abiria 30 mpaka 40 mabaharia wavuvi.

Je, ni vyombo vya aina gani unavyokusudia kuwaletea wavuvi, ikiwa Zanzibar ni kisiwa na vile vile kina wavuvi wengi? Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kwa takwimu za haraka haraka kujua wapi na wapi, wizara imetoa vitu vingi na sehemu nyingi kwa kuwa takwimu hizo sasa hivi sinazo, basi naomba nikuletee kwa maandishi hata kesho asubuhi.

Lakini kuhusu bahari kuu, wizara yangu imejitahidi hivi sasa na iko katika bajeti ya serikali kununua meli moja kubwa ili kuwafunza vijana wetu 30 kuelekea huko, na kwa kuanzia tutaanzia na vijana wa *form IV* kwa sababu tunahitaji kuwa na uvuvi wa kisasa na meli yenyewe itakuwa ni ya *electronic* kuweza kuwafundisha vizuri sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, lakini vizuri umpatie keshokutwa *Inshaallah,* sio kesho, kesho ni skukuu kwetu.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi ya kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ina mpango wa kununua meli na kwenda uvuvi wa bahari kuu umeupanga zamani sana, na hadi hivi sasa tumeambiwa iko kwenye mipango.

Je, wizara yako ni lini itaukamilisha mpango huo ili wananchi wapate kufaidika katika nchi yao?

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu hivi sasa imejipanga vizuri na wakati wowote hali ya fedha ikiruhusu tutaweza kufanya mpango huo ili kuona basi wananchi wa Zanzibar hii wanafaidika na programu hiyo ambayo tumeiandaa vizuri.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia fursa ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa azma ya serikali ni kupunguza umaskini na kuwaongezea wananchi wake kipato, na kwa kuwa bahari kuu kila siku tunapiga kelele kama serikali inajipanga kwa ajili ya kuzalisha uvuvi wa bahari kuu ili kuwapatia wananchi ajira na kuwapunguzia umaskini.

Mhe. Naibu Waziri ametuambia kwamba serikali iko mbioni kujipanga ili kupata meli japo moja ya kuanza kufanya hiyo kazi ya uvuvi wa bahari kuu. Napenda kumuuliza Mhe. Naibu Waziri, kwa sababu uvuvi huu wa bahari kuu anasema anataka uvuliwe kitaalamu, na inategemewa kwamba watakaoanzisha ni kuanzia *form IV* na kuendelea.

Sasa namuuliza Mhe. Naibu Waziri, hao watakaoanza kama watu 30 wanasoma chuo gani?

Kwa kuwa Zanzibar hatuna Chuo cha Uvuvi na wakati tunaelekea kwenda kuvua uvuvi wa bahari kuu ni lini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaona haja ya kuanzisha Chuo cha Uvuvi ili wananchi wapate kuvua kwa uadilifu na kwa uvuvi wa kisasa wa kitaalamu?

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti,

a) Wizara yangu kweli haina chuo, lakini tayari tumeanza kuishauri mitaala iingie katika vyuo vya *Vocational Training* yaani Vyuo vya Amali ili basi kuweza kuona wananchi wetu wanapatiwa mafunzo maalum ya kuweza kuvua bahari kuu.

Vile vile hali itakaporuhusu nadhani tutaipata meli hii na tutawachukua pale, lakini isitoshe kwa sasa tunashirikiana na Chuo cha Mbegani Tanzania Bara, ili kuona basi tunaandaa vijana wetu na kweli meli ile ile kutakuwa na wakufunzi ambao

ndio watakwenda kuwafundisha kwenda katika maji ya kina kirefu na tuache mazoea ya kuvua kwa upondo kama tulivyozowea, ili tuweze kukaa masaa 24, wiki moja na hadi mwezi katika ile bahari kuu tuitumie ipasavyo.

Nam. 30

Kukosekana Huduma ya Umeme Katika Kijiji cha Matuuni

Mhe. Salim Abdalla Hamad - Aliuliza:-

Wananchi wanaoishi katika kijiji cha Matuuni, Shehia ya Piki, Jimbo la Mtambwe wamejitahidi katika kupatiwa nishati ya umeme na hivi sasa wameshafanikiwa kupata nguzo za umeme 26 ambazo zinatosheleza kwa kupatiwa huduma hiyo.

(a) Ni sababu zipi za msingi zilizosababisha Wizara kushindwa kuwapatia wananchi huduma hiyo muhimu.

(b) Hivyo ni sawa kwa Wizara kutotoa kipaumbele kwa wananchi hawa kusaidiwa baada ya kuonesha juhudi zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 30 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, wizara inatoa shukrani kwa Uongozi wa Jimbo la Mtambwe kwa kuchangia baadhi ya vifaa vya kuwasogezea huduma za umeme wanakijiji wa Matuuni Shehia ya Piki.

Mhe. Mwenyekiti, kazi ya kupeleka huduma ya umeme katika kijiji cha Matuuni imeshakamilika tokea tarehe 09/08/2013, na

tayari Msikiti wa Matuuni unatumia huduma hiyo ya umeme. Aidha, baadhi ya wananchi wa kijiji hicho nao wameshaanza kujengewa *service line* katika nyumba zao.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikubaliane na Mhe. Naibu Waziri kwamba ni kweli huduma ya umeme katika kijiji hiki imeshafika. Swali langu ni kwamba ni sababu zipi za msingi zinazosababisha wizara kushindwa kuwapatia wananchi huduma hiyo muhimu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu na hapa ilishindwa, tulichangia nguzo wenyewe na hatua ya pili tukatakiwa tutoe shilingi milioni 13 na tukatoa. Kutokana na swali langu mama, baada ya gharama zote hizo. Je, wizara iligharamika kiasi gani katika kupeleka umeme pale Matuuni. Hilo ni swali la mwanzo.

Swali la pili kwa sababu ulikuwa umeme haujaenea na sasa hivi inahitajika kiasi cha shilingi 600,000 kumaliza kazi katika kijiji kile. Je, Mhe. Waziri hatoona huruma baada ya juhudi zetu zote tulizochukua kutusaidia kwa hizi shilingi 600,000 ili kuongeza umeme katika kile kijiji kwa sehemu ambazo bado hazijapata.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza hapo awali kwamba huduma ya umeme ndani ya kijiji cha Piki tayari imeshafikia, kilichobakia ni kwamba wananchi wenyewe kufuatilia katika Shirika la Umeme kwenda kuomba usajili na kuunganisha ndani ya majumba yao.

Suala la pili ni kwamba kuhusiana na mchango alioutoa, ni kweli kwamba wametoa mchango wao na tumewashukuru katika mchango huo walioutoa, lakini mchango wao walioutoa haukutosheleza kuikamilisha huduma hiyo ya umeme, isipokuwa Shirika langu la umeme kwa kuongeza nguvu zake pamoja na michango yake, ndio ikakamilisha ujenzi huu wa *line* ya umeme ndani ya kijiji hicho cha Piki.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri, lakini kwanza Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii ya kumpongeza sana Meneja wa Shirika hili kwa kazi nzuri za kusaidia wananchi wa vijijini kwa njia ya mkopo. Swali langu liko hapa.

Mhe. Naibu Waziri hivi karibuni nilisikia nguzo zilikuwa hazipo. Je, hivi sasa nguzo zimeshakuja?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba nguzo ndani ya Shirika letu la Umeme kwa kipindi hiki hatuna, lakini nguzo hizo tumeshaagiza na wakati wowote zitawasili hapa Zanzibar. Kama tunavyoelewa kwamba Zanzibar hatuna uzalishaji wa nguzo, isipokuwa lazima tuagizie nje ya nchi hii, ili kuziwasilisha Zanzibar. Kwa hivyo, tumeshaagiza nguzo hizo kutoka Afrika ya Kusini na wakati wowote zitawasili Zanzibar na zikifika Zanzibar tutazisafirisha kuzipeleka Pemba kwa matumizi ya wananchi wa Pemba pamoja na wananchi wa Unguja.

Mhe. Farida Amour Mohamed: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri katika majibu yako umekiri kwamba kijiji ambacho tayari kimeshafika umeme ni wanakijiji wenyewe kufikisha ndani ya majumba yao, na kuna baadhi ya watu katika maeneo mengi wanalalamika kuwa tayari wameshalipia, wameshamaliza huduma zote na bado hawajafikishiwa.

Je, unaweza kuniambia kuwa baada ya mtu kukamilisha huduma zote zinazotakiwa kwenye Shirika la Umeme, inachukua muda gani kupatiwa huduma hiyo ahsante?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba ziko kasoro ndogo ndogo

kwa Shirika letu la Umeme kwamba baadhi ya wananchi wanapolipia huwa wanachelewa. Lakini sio makusudio ambayo yanakusudiwa rasmi kwamba kuwachelewesha wananchi hawa, isipokuwa Shirika la Umeme lina utaratibu maalumu wa kuwaunganishia wananchi umeme. Baada ya kujaza fomu, fomu hiyo inatakiwa watoke watu wetu wa *service line* kwenda kuangalia ndani ya maeneo yao, baada ya kuangalia na kupima halafu tuwafanyie hesabu na hatimaye tunawataka wananchi hao walipe. Baada ya kwishakulipa tunachokiangalia zaidi ni kwamba yule mteja aliyefuatiliwa mwanzo basi ndiye tunayemuunganishia umeme mwanzo, hatimaye ndio anafuatia aliyekuja ndani ya kipindi cha pili.

Kwa hivyo, niwaombe wananchi kwamba wastahamili na shirika letu liko makini na liko tayari kuwahudumia wananchi wake ipasavyo. Hatuna muda maalumu isipokuwa lengo ni kuwasambazia wananchi ndani ya vijiji vyote vya Zanzibar.

Nam. 6

Mali za Bi Kidude Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabla ya kujibiwa swali langu nambari 6 linalohusu Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, inayoongozwa na *engineer* Mhe. Said Ali Mbarouk. Nitakuwa sijamfanyia haki kwa kumsifu akiwa na pumzi zake na mimi nikiwa na pumzi zangu. Wengi wetu humsifu mtu akishakufa kuwa alikuwa mzuri.

Mhe. Said Ali Mbarouk nikupongeze kwa dhati kabisa kwa kazi unayoifanya, ikiwa hujali usiku wala mchana, wala jua wala mvua na hii imetokana na umakini wako katika kipindi kifupi tu ulichoongoza wizara mbili. Naamini mimi katika ndoto zangu wakati wote Dk. Ali Mohamed Shein alipofanya mageuzi,

Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano inakunukia kutokana na sifa za *engineer* ulizokuwa nazo.

Mhe. Mwenyekiti, waziri huyu ameonesha uwezo mkubwa katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa na kuokoa nguvu za vijana kazi, na kufurahisha wengi na kuudhi wachache, mategemeo yake mengi atayapata kwa Mwenyezi Mungu, akiwemo Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba swali langu nambari 6 lijibiwe.

Mwezi wa Aprili mwaka huu Taifa limepata msiba mkubwa kwa kuondokewa na msanii mkongwe Bi Kidude.

(a) Kutokana na kazi hiyo aliyofanya kuwa kivutio kikubwa kwa Watalii na Watafiti wa mambo ya muziki, kwa nini nyumba yake isiingizwe katika makumbusho ya Taifa pamoja na kazi alizofanya wakati wa uhai wake.

(b) Serikali imetoa mchango gani katika kumuenzi msanii huyo baada ya kufariki.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 6 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, Serikali imejipanga kuzienzi kazi za usanii zilizoachwa na Marehemu Msanii Mkongwe Bi. Kidude binti Baraka. Katika kufanya kazi hiyo, tutajitahidi kukusanya kazi zilizofanywa na msanii huyo na kuzihifadhi kwenye maktaba zetu na kuzitumia hasa tutakapokuwa katika maadhimisho ya kuwaenzi wasanii

mashuhuri wa Zanzibar ambayo yamekuwa yakifanyika kila mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu nyumba ya msanii huyo kuigeuza kuwa ni makumbusho ya Taifa. Hilo ni wazo zuri, lakini linahitaji likubaliwe na warithi wa msanii huyo ambao sasa ndio wamiliki wa nyumba hiyo.

(b) Mhe. Mwenyekiti, mchango uliotolewa na serikali wa kumuenzi msanii huyo baada ya kutokea kifo chake, ni kusimamia kikamilifu maziko yake pamoja na kumuombea dua. Mhe. Mwenyekiti, huu ni mchango pekee uliobakia wa kumuenzi ambao ulihitajika kutoka kwa wenzake waliobaki duniani. Mungu amlaze mahala pema peponi - Amin

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri. Je, serikali ina mpango gani wa kuhifadhi kazi alizozifanya Marehemu Bi Kidude, ikiwemo kuziingiza katika kumbukumbu za Sanaa na Utamaduni na ukizingatia Marehemu huyu amefanya kazi Afrika na Barani Ulaya.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, swali lake nimelifafanua vizuri, kwa sababu nilisema kwamba Msanii huyu tutamuenzi na kazi zake zitawekwa kwenye maktaba zetu ambazo zipo Rahaleo.

Mhe. Mwakilishi nakuomba sana tukiwa pamoja na wewe tushirikiane ili kuimarisha usanii.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa ruhusa na mimi kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba na mimi nimuulize kama ifuatavyo. Kwa kuwa wasanii ni watu muhimu sana katika jamii kwa ajili ya kuelimisha na kutoa burudani.

a) Je, ni lini hasa serikali itawaenzi wasanii hasa wale wanaostaafu, kwa kuonesha zile sanaa zao ambazo walikuwa wakizifanya, jambo ambalo lingewajengea sifa wasanii hawa, lakini pia kuweza kuacha historia nzuri katika nchi yetu.

b) Kama sanaa hizi zinaenziwa zipo, ni kwa nini hatuoneshwi sanaa za wasanii wakongwe. Kwa mfano Suwedi Mabugira ambao waliweza kuonesha sanaa nzuri, ili tukaweza kujikumbusha ile michezo yao ambayo ilikuwa na mantiki nzuri?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba Mzee Bakari Abeid ni msanii mkongwe na tulikuwa tunazitoa taarifa zake sahihi za usanii, akaja mwanawe akatuletea barua akasema hataki atolewe mzee wake kwenye vyombo vya televisheni.

Mhe. Mwakilishi nataka nikuambie mtu akiwa ana familia yake, basi ni mpaka familia yake ikubali ndipo tunazitoa tasnia zake kwenye TV.

Vile vile Mhe. Mwakilishi nataka nikuambie wasanii wakongwe tunawaenzi na vikundi vya usanii tunavienzi na sasa hivi nataka nikuambie vikundi hivyo vitaingia kwenye sherehe za miaka 50, wasanii wote wa Zanzibar na wasanii wakongwe waliopo.

Mhe. Mwakilishi ukiwa ni mwanamke mwenzangu nakuomba sana uhamasike na vipindi vyengine ambavyo vinatokana na usanii wa utamaduni wa Kizanzibari wa mavazi na mambo mengine na tukiwa pamoja na wewe nakuomba sana tushirikiane ili tuandae vipindi hivyo ili Wazanzibari wavione.

Nam. 7

Vyombo vya Habari vya SMZ Kukosekana Bungeni

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Aprili mwaka huu Kikao cha Bajeti kilianza Dodoma lakini vyombo vya habari vya SMZ havionekani vikirusha matangazo kutoka Dodoma na kuwanyima haki wananchi wa Zanzibar ya kupata habari kupitia vyombo vyao vya serikali kinyume na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ambayo inatoa haki ya wananchi kupata habari.

(a) Je sababu gani zilizopelekea vyombo vyote vya SMZ vinashindwa kutuma waandishi na watangazaji kuripoti shughuli za Bunge.

(b) Kama tatizo ni fedha kwa nini serikali isiitishe kongamano la kuchangia vyombo vya habari vya serikali ili waweze kwenda kuripoti vikao kwa maendeleo ya Zanzibar.

(c) Kukosekana kwa watangazaji na waandishi kutoka Zanzibar na badala yake kutegemea vyombo vya Tanzania Bara kunasaidia vipi hoja za Zanzibar kupewa uzito wake.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na suala hili lilivyo Mhe. Naibu Waziri ameniomba leo hakuwa tayari kulijibu. Naomba liondoke kwenye *order paper* mpaka siku nyengine litakapopangwa. Kwa hivyo, kwa siku ya leo naliondoa nasubiri uamuzi mwengine wa Baraza.

Mhe. Mwenyekiti: Umeondoa swali au?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri kaniomba leo hili swali litakuwa halina jawabu. Kwa hivyo, naomba kuliondoa.

UTARATIBU

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, muuliza swali hapa Mhe. Jaku Hashim Ayoub kasema kwamba serikali imemuomba kwamba aondoshe swali. Tafsiri yake ni kwamba serikali imeshindwa kutoa jawabu, kitu ambacho katika serikali inayowajibika kwa pamoja haiwezekani serikali kushindwa na jawabu. Kwa hivyo, naomba swali lake lisiondoshwe na serikali ijibu swali hilo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. Serikali ya Mapinduzi ya Awamu ya Saba inayoongozwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein, iko tayari kujibu swali hilo.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, swali lililoulizwa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub, tulimpa nafasi ya kusema kwamba swali lake anataka liulizwe au laa, lakini Mhe. Jaku Hashim Ayoub alichokizungumza anaelewa mwenyewe namna alivyofahamu, lakini kimsingi mwenye uhalali wa kusema kwamba swali lake lijibiwe au lisijibiwe ni yule mwenye kuuliza swali mwenyewe. Sasa kama mwenyewe ameridhika kwamba anahisi kuwa swali lake lisijibiwe nahisi tuendelee na utaratibu mwengine. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa utaratibu na kanuni, ikiwa Mhe. Mjumbe ametaka swali lake lisijibiwe ina maana kwamba halitokuja tena katika maswali kwa sababu yeye mwenyewe ameshakubali lisijibiwe, serikali ipo tayari kujibu, akisema kwamba lisijibiwe ina maana lisije tena kwa mara nyengine. Nakushukuru.

Nam. 36

Ujenzi wa Chuo cha Kufundisha Madaktari Pemba

Mhe. Abdi Mossi Kombo - Aliuliza:-

Katika kukuza maendeleo na kupunguza matatizo ya kupata wataalamu wazuri wa afya Unguja na Pemba na katika kupunguza sana gharama za usafiri wa wanafunzi wanaotoka Pemba kuja Unguja kufuata mafunzo ya afya.

Je, ni lini Wizara ya Afya itaanzisha kituo cha kusomeshea madaktari Kisiwani Pemba?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 36 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, miaka iliyopita palikuwa na jaribio la kufungua Tawi la Chuo cha Afya Pemba ili kufundisha manesi ambao ndio kada yenye upungufu mkubwa hasa kwa Pemba.

Nia na madhumuni ilikuwa ni kama ifuatavyo:-

1. Kuongeza idadi ya wafanyakazi wa kada hiyo.
2. Ingawa muajiriwa wa afya anatakiwa afanye kazi popote nchini, lakini hili lingesaidia kwa kiasi fulani kuweza kuwabakisha wale wanafunzi wenye asili ya Pemba kwa sababu wao wapo nyumbani kuliko kumpeleka mfanyakazi aliyetoka Unguja.
3. Wanafunzi wanaotoka Pemba wakisoma Unguja baada ya miaka minne imeonekana maisha yao yanabadilika na huwa hawataki kurudi kusaidia nyumbani, na hata wakiwa wamekuja kwa ufadhili

wa kijiji alichotoka, hilo wanalisahau na wanang'ang'ania kubaki Unguja bila ya kujali shida zilizofanya kijiji chake kumlipia ada ili aweze kurudi kuwasaidia.

4. Pia baadhi ya wanafunzi wanaotoka Unguja wangeweza kubaki Pemba kwa hiari baada ya kuishi kwenye mazingira ya huko kwa kuyapenda au kuolewa.

Mazingira ya wakati huo yaliyofanya kuwepo kwa jaribio hilo ni kama yafuatayo:-

Mazingira chanya ambayo yangewezesha tawi hilo kufunguliwa, wakati huo Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii zilikuwa pamoja. Kwa hivyo, wizara ilipata jengo moja la ustawi wa jamii katika mji wa Chake Chake karibu na Uwanja wa Gombani na eneo lilikuwa kubwa, ambalo lingeweza kujengwa majengo mengine kwa mahitaji ya chuo.

Pia kuna Hospitali kubwa ya Chake Chake ambayo ingetumika kwa ajili ya kufundishia na nyenginezo nyingi kwa ajili ya mazoezi ya kujifunza kwa vitendo.

Vile vile kulikuwa na mazingira hasi ambayo yalifanya nia hiyo ishindikane, kwa sababu kulihitajika fedha nyingi kwa ajili ya kujenga majengo mengine ya kufundishia, dakhalia, nyumba za walimu, mkahawa na maabara ya kufundishia na hayo yanagharimu fedha nyingi ambazo hazikuwepo.

Isitoshe kwa wakati huo hata hicho Chuo cha Afya cha Mbweni kilikuwa bado hakijakamilika kujengwa. Pia kulikuwa kunahitajika gharama za uendeshaji na fedha za nauli na posho za walimu ambao walikuwa wanatakiwa waende Pemba na kurudi kwa zamu, kwa sababu kuanzia isingewezekana kupata walimu wa kudumu kwa matawi yote mawili.

Kwa hali ya sasa ambapo Chuo cha Afya kinaelekea kuwa Tawi la *SUZA* maamuzi hayo kwa upande wa Wizara ya Afya hatuna tena.

Mhe. Abdi Mossi Kombo: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa ruhusa yako naomba kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Naibu Waziri wa Afya.

Kutokuwa na kituo cha kufundishia madaktari Pemba, serikali haioni kwamba kuwaleta wanafunzi Unguja itakuwa inaleta usumbufu sana kwa wanafunzi hao ambao wengine itakuwa hawana sehemu za kuishi?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi ambacho Vyuo vya Afya tangu vilipoanza mpaka hii leo wanafunzi wanaotoka Pemba wanakuja Unguja na wala hatujawahi kupata malalamiko.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa wanafunzi wanaosoma Chuo cha afya Mbweni kutoka Pemba wengine wanatoka katika Jimbo la Mtambwe na mimi ndiye mwakilishi wao, kwa sababu huwa mara zote wanasaidia kwa kadri ninavyoweza kutokana na matatizo wanayoyapata kimazingira kutoka Pemba kuja Unguja kwa ajili ya kuweza kuishi na hasa pa kukaa. Hivyo, haoni Mhe. Waziri kama upo uwezekano angefikiria sana swali mama alilouliza na Mhe. Abdi Mossi Kombo, ili na kule Pemba tupate hichi kituo? *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, nimejibu kwenye swali la msingi kwamba kwa gharama hizo tawi la pili Pemba haliwezekani kufunguliwa, na hivi sasa chuo kiko chini ya *SUZA*. Kwa hivyo, muje muiombe *SUZA* ifungue tawi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, serikali imefanya utafiti wa kiasi gani wa kuamua Chuo cha Afya kuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha *SUZA* badala ya chuo hicho kujitegemea, kwa sababu tumeona mfano hai wa Chuo cha Ualimu Nkurumah kuondoshwa na hivi sasa mporomoko wake kuhusu walimu unavyoendelea.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Mjumbe na analolisema kwamba Wizara ya Elimu walifungua Chuo cha Ualimu Nkurumah, lakini mahitaji ya Wizara ya Elimu ni tofauti na mahitaji ya Wizara ya Afya, kwetu sisi bado suala hilo ni mzigo. *(Makofi)*

Nam. 49

Matengenezo Barabara ya Mkarafuu Mmoja – Kiuyu

Mhe. Salim Abdalla Hamad – Aliuliza:-

Serikali kupitia wizara hii inastahiki pongezi kwa kutumia fedha nyingi kujenga upya daraja la Shangafu na kuvunja daraja la zamani ambalo lilikuwa bovu na lenye kuhatarisha maisha.

Ni lini serikali itaijenga barabara ya Mkarafuu Mmoja – Kiuyu, ili iweze kupitika ipasavyo na kusaidia sana wananchi wa vijiji vya Shengejuu, Mashuga, Tondooni na Kiuyu ambao ndio watumiaji wa barabara hiyo na hasa kutokana na kuwa daraja ambalo lilikuwa ni kikwazo tayari limeshajengwa na linatumika.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 49 kama ifutavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, suala la ujenzi wa barabara hasa barabara za ndani ni jukumu ambalo wenzetu wa Halmashauri wanawajibika moja kwa moja.

Hata hivyo, pamoja na jukumu la msingi la Mfuko wa Barabara wa Kuzitunza na Kuziendeleza Barabara zetu ili zibakie salama bado tumeona ipo haja maalumu ya kuona taasisi hii inashirikiana na wizara yetu katika ujenzi mpya wa miradi ya miundombinu ikiwa ni pamoja na barabara na madajara kama ilivyo kwa barabara hii ya Mkarafuu Mmoja hadi Kiuyu kwa kuanzia na ujenzi wa daraja la Shangafu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo mafupi, sasa naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, wizara imepokea pongezi za Mhe. Mwakilishi kwa kutambua juhudi zetu za ujenzi wa daraja la Shangafu. Kutokana na umuhimu wa barabara ya Mkarafuu Mmoja hadi Kiuyu, wizara kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara iliamua kulijenga upya daraja la Mkarafuu Mmoja ili kwa kuanzia barabara hiyo iweze kupitika na kuwaondolea usumbufu wananchi wanaoitumia barabara hiyo.

Baada ya kukamilika kwa ujenzi wa daraja hili, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imepanga katika mwaka wa fedha 2014/2015 kuingiza kwenye bajeti ya fedha za Mfuko wa Barabara, barabara hiyo kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha kifusi.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na pongezi kubwa kwa Mhe. Naibu Waziri kwa kusema kuwa tutaingia katika bajeti ya mwakani. Lakini kwa sababu hivi karibuni kwa kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo tuliifanyia *grading* barabara hii na ikawa inapitika lakini hatukuwa na uwezo wa kutia hicho kifusi. Kwa vile mvua iliponyesha imeshaanza kuharibika na hali inarudia vile vile.

Je, haoni kuwa upo umuhimu wa kutusaidia angalau kwa zile sehemu ambazo hazipitiki kwa siku za mvua zikatiwa kifusi na kusubiri mpaka hapo mwakani serikali itakapokuwa na uwezo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, maelezo ya Mhe. Mjumbe tumeyaelewa vizuri na wizara yetu kwa mwaka huu nguvu na bajeti yetu tulikuwa tumekusudia ujenzi wa daraja kwa kutambua kwamba daraja lile likikamilika tutakuwa tumekamilisha kiungo muhimu kwa watu wanaotoka upande mmoja kwenda upande wa pili. Vile vile ni kweli kwamba kuna baadhi ya maeneo ambayo yamewekwa kifusi na kama ilivyo kawaida imekuja mvua imeweza kuondosha kile kifusi.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Mwakilishi kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba yeye mwenyewe binafsi, Halmashauri husika na kama ilivyo kawaida kwamba sisi tuko tayari kutoa msaada wa vifaa, vitendea kazi pamoja na mafundi wetu na gharama zinazostahiki watusaidie wao, ili twende tukaweze kufukia maeneo hayo na kuweza kufanya urahisi wa watumiaji wa barabara husika.

Lakini kuji-*commit* moja kwa moja kwamba sisi kama wizara tutatia kifusi kwa kipindi hichi hatuna eneo ambalo tunaweza kupata hizo fedha za kufanyia huduma hiyo, isipokuwa vifaa na wataalamu wetu tuko tayari kuwatoa muda wowote kwenda kufanikisha huduma hiyo muhimu ya kuziba maeneo hayo ambayo hayapitiki.

Nam. 100

Adhabu ya Kifo Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Kwa muda mrefu utekelezaji wa adhabu ya kifo umekuwa mgumu nchini kutokana na Marais kutosaini adhabu hizo na kuwafanya wahusika kuishi katika mazingira ya wasiwasi bila ya kufahamu hatima yao.

(a) Kama Marais wamekuwa wazito kusaini hukumu hizo, serikali ina mpango gani wa kufuta adhabu hiyo kama utekelezaji wake umekuwa mgumu?

(b) Kuendelea kuwaweka magerezani watu waliohukumiwa kunyongwa bila ya utekelezaji wake kufanyika sio uvunjaji wa haki za binadamu?

(c) Kwa nini Marais wanakuwa wazito kusaini hukumu hizo za kifo wakati wameapa kulinda Katiba na Sheria?

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 100 lenye (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, adhabu ya kifo hutolewa na mahakama baada ya kusikiliza kesi ya mauaji au kesi nyengine yoyote ambayo imeainishwa kuwa adhabu yake ni kifo, na kujiridhisha kwamba mtuhumiwa kwa ushahidi usio na shaka yoyote ile ametiwa hatiani kwa kosa hilo la mauaji, ambalo adhabu yake imeelezwa kwenye vifungu husika vya Sheria ya Adhabu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa hukumu zinazotolewa na mahakama hukatiwa rufaa, hivyo utaratibu wa kutekeleza Hukumu ya Mahakama huchelewa kutokana na kusubiri maamuzi ya rufaa ya Mahakama za Juu.

Mhe. Mwenyekiti, suala la serikali kuendelea na utamaduni wa kutoa adhabu ya kifo limejadiliwa sana kwenye makongamano tofauti, ambapo kuna baadhi ya Wasomi na Wanaharakati wamekuwa mstari wa mbele kutoa maoni na mawazo ya kuachana na adhabu ya kifo, na pia wapo baadhi ya wasomi na wananchi wengi ambao bado wana hoja za msingi za kutaka adhabu ya kifo iendelee kutumika nchini.

Umoja wa Mataifa katika kikao chake cha Oktoba 2012 kilizungumzia sana suala hili lakini haukupatikana uamuzi wa moja kwa moja. Sababu kubwa ni kuwa baadhi ya nchi wana ushahidi kuwa adhabu ya kifo inapunguza uhalifu.

Kwa mfano, Tanzania Bara baada ya kutoa adhabu ya kifo watu wanao wahujumu maalbino, matatizo hayo yamepungua sana, lakini Marekani na Nigeria walipoweka adhabu ya kifo kwa makosa ya ujambazi inaonesha kuwa uhalifu bado unazidi. Nchi nyengine ni suala la kidini na huwa halina mjadala, na kwa siku hizi biashara ya unga na dawa za kulevya nazo zimeekewa adhabu ya kifo kwa nchi nyingi duniani.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa hoja zinazotolewa na wanaotaka adhabu ya kifo iondoshwe na wale wanaotaka adhabu hiyo iendelee kutekelezwa, serikali inachambua hoja zote kwa makini kabla ya kutoa maamuzi ambayo yatakubalika na jamii yote ya Wazanzibari.

Bado Wazanzibari wana nafasi kubwa ya kutoa maoni juu ya adhabu hii; je kweli ni adhabu inayopunguza uhalifu (yaani *deterrence*) au ni vyema kumuonya mtu na kuwapa onyo wengine wasitende

kosa kama hilo. Haya ni mambo ya kuzingatiwa kwa makini sana na baadae kuishauri serikali, ili iweze kuamua kwa uhakika kuwepo au kutowepo kwa adhabu ya kifo.

Mhe. Mwenyekiti, kumbukumbu zinaonesha kwamba hakuna Rais wa Zanzibar ambaye ametia saini amri ya adhabu ya kifo. Marais wote waliotangulia wamekuwa wakitumia uwezo wao wa Kikatiba wa Msamaha ama wa kutoa Msamaha bila ya Masharti au kwa masharti kwa mtu yeyote aliyehukumiwa kwa kosa lolote, kutoa uakhirisho ama kwa muda au wa moja kwa moja katika utekelezaji wa adhabu yoyote iliyotolewa na Mahakama kwa mtu huyo kuhusiana na kosa alilotenda, ama kubadili adhabu aliyopewa mtu kutokana na kosa lolote na kuifanya iwe ndogo zaidi. Uwezo huu wa Rais upo chini ya kifungu cha 59 cha Katiba ya Zanzibar.

b) Kesi zinazohusu adhabu ya kifo ni nzito. Ni vyema muhusika akapewa nafasi kubwa ya kukata rufaa na kesi yake ikachunguzwa kwa makini, ili ihakikishwe kuwa kweli mtuhumiwa amefanya kosa hilo na anastahiki kunyongwa. Kwa maana hiyo mtuhumiwa huyo kukaa gerezani kwa muda si kuvunja haki ya kibinaadamu bali ni kutekeleza masharti ya Katiba kwa kumpa haki mtuhumiwa, ili aridhike na aone kama haki inatendeka.

c) Marais wengi duniani huwa wazito kusaini hukumu za kifo kwa sababu ya kutaka kujiridhisha zaidi.

Pili, Rais ndiye kiongozi wa nchi, na mtuhumiwa ni raia wake. Sawa sawa kwa mzee na mtoto wake anapofanya kosa, anaweza kumpa msamaha wa kosa hilo pamoja na kumuwekea masharti fulani. Lakini

pia anaweza kuipunguza adhabu aliyokuwa ampe na kuifanya ndogo zaidi kwa masharti au bila ya masharti yoyote.

Kwa hivyo, marais hutumia busara hiyo nzuri katika kujiridhisha na kumuwezesha yeye au kuidhinisha adhabu hiyo ya kifo au kutoa adhabu nyengine yoyote ambayo anahisi ingefaa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kutojibu swali la msingi naomba nimuulize swali moja dogo tu la nyongeza. Serikali itachukua muda gani kuchambua hoja zote zilizojitokeza na kutoa uamuzi kuhusu adhabu ya kifo?

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, serikali itategemea maoni ya wananchi, sasa ikiwa wananchi watakapotuletea maoni yao kwa haraka basi na serikali nayo itafanya suala hili kwa haraka. Lakini napenda nimueleze Mhe. Mjumbe kwamba suala hili si tatizo kwa Zanzibar tu, isipokuwa ni tatizo kwa nchi zetu za dunia yaani nchi zote zina mirengo miwili; wengine wanasema adhabu ya kifo iwepo na wengine wanasema isiwepo.

Vile vile kama nilivyosema kwamba mwaka jana tulikuwa katika mkutano huo unaohusiana na adhabu ya kifo, lakini bado Umoja wa Mataifa haukutoka na *solution* katika suala hili bado waliachiwa kila nchi wajaribu kuendeleza hayo mawazo na maoni kutoka kwa wananchi wao, ili iwezekane, lakini lengo ni kwamba adhabu ya kifo hatimaye iweze kuondolewa lakini hatujafikia hapo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, ninayo mambo mawili kwanza naomba nitoe hoja, pili naomba niweze kuuliza swali kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, haoni kwamba ipo haja hivi sasa sheria mukaitengeneza na ikatamka rasmi badala ya kusema mtu kunyongwa na mkaweka bora mtu afungwe maisha. Hilo ndio swali langu.

Lakini kabla ya kujibiwa naomba nimalizie na hoja yangu, ili niweze kujibiwa vizuri. Hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, naomba tuweke Kanuni kando kwa kuwa leo ni siku ambayo sisi wengine tunajitayarisha kwa kupata kusheherekea siku ya Sikukuu, basi Kanuni iwekwe kando tusirejee tena jioni kwa ajili ya kujitayarisha ikiwemo kununua vitu. Kwa hivyo, kuhusiana na hilo Mhe. Mwenyekiti nimeona nitoe hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, hoja yako itazingatiwa. Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, naomba nijibu, swali la pili kwamba hilo si kazi yangu isipokuwa ni kazi ya Mwenyekiti. lakini swali lake la kwanza.

UTARATIBU

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nilisema hivi *options* zangu ni mbili kwamba hii moja Mhe. Mwenyekiti nimeelekeza Kiti kwako wewe hoja na nikasema ninatoa hoja kwako wewe kwenye Kiti.

Pili ndio nikasema hili namuwekea Mhe. Waziri kwanza asiweze kunijibu mpaka nikatoa hoja yangu kukuelekeza wewe, na hili sitaji anijibu yeye Mhe. Waziri, kwa sababu hajawa na kiti cha Mwenyekiti. Kwa hivyo, naomba anijibu hili kwa mujibu wa sheria ambapo wizara yake itaweza kututengezea sheria. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, tumesema kwamba hoja yako itazingatiwa. Mhe. Waziri tuendelee.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, swali lake anasema kwamba tuweke sheria ambayo inasema kwamba tuondoe suala la kunyongwa na mtu afungwe maisha.

Kwa hivyo, kama nilivyosema mwanzo kwamba haya ni mambo ambayo yanazungumzwa na wala hatuwezi kuweka sheria hii mpaka jamii tuwe na suala moja, kwa sababu kuna mambo mengi humu. Kwa mfano, kuna sheria za kidini na nyengine si za kidini.

Sasa tunasema kwamba tuondoe suala la kunyongwa na afungwe maisha ina maana tumeshakata kwamba hivi sasa adhabu ya kifo haipo je jamii inasema hivyo, nadhani ni vyema tuisikilize jamii kwanza; kwamba wanasema bado iwepo adhabu ya kifo au isiwepo.

Vile vile baadhi ya jamii wanasema kwamba adhabu ya kifo iwepo kwa sababu inapunguza na kuleta khofu kwamba wewe ukifanya uhalifu huu kama vile ukimuua na wewe utauliwa, angalau watu wanaogopa, lakini ukisema kwamba hakuna adhabu ya kunyongwa na mtu afungwe maisha, basi wengine wanasema unazidisha uhalifu. Kwa hivyo, ni masuala ya kuzungumza kwa pamoja na baada ya kuzungumza ndio jamii inaweza ikaja na uhakika kwamba sasa adhabu hii iwe hivi au kwa utaratibu huu.

Kutokana na hali hiyo, bado tunaiachia jamii, *NGO's* zinazohusika pamoja na wanaharakati, na pale ambapo tukimaliza masuala hayo na watakaposema, basi sisi tutaiweka katika sheria kwa mujibu wa jamii itakavyosema.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kampuni ya Mwaka 2012

(Kusomwa kwa Mara ya Pili)

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa Mswada wa Sheria ya Usajili wa Kampuni na mambo mengine yanayohusiana na hayo usomwe kwa mara ya pili.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Katiba na Sheria kupitia Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali inaendelea na Mpango wa Kuimarisha Mifumo ya Usajili, ili kurahisisha kazi za usajili kwa kuweka sheria bora zitakazosaidia kuleta ufanisi katika utoaji wa huduma za usajili kulingana na maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Mpango huu unatekelezwa kwa kuzingatia mahitaji ya wakati, walengwa, ukuaji wa ushindani wa kibiashara na pia kuzingatia mazingira ya sasa yanayoifanya dunia kuwa kijiji kidogo katika maingiliano ya kibiashara.

Katika utekelezaji wa mageuzi haya wizara imeona ipo haja ya kuipitia na kuitunga upya Sheria ya Usajili wa Kampuni, ili ikubaliane na mageuzi ya mfumo mzima wa usajili wa kampuni hapa Zanzibar. Mageuzi yanalenga kuondoa kasoro zilizokuwa zikijitokeza katika uendeshaji wa biashara za kampuni.

Mhe. Mwenyekiti, Sheria ya Usajili wa Kampuni (*Companies Decree*) sura ya 153 iliopo sasa inatokana na Sheria ya Kampuni ya Uingereza ya mwaka 1948 (*English Companies Act* ya mwaka 1948). Sheria hiyo imefanyiwa marekebisho mengi na ilifanya mageuzi makubwa mwaka 1985 na baadaye yakafuatiwa na marekebisho mengine yaliyopelekea kuwa na sheria mpya katika mwaka 2006.

Kutokana na kasi ya mabadiliko, sheria hiyo sasa haiendani na wakati na utaratibu, vigezo na mifumo ya kimataifa, vile vile haitoshelezi mahitaji ya sasa ya kibiashara yanayokwenda sambamba na sayansi na teknolojia. Katika hali hiyo inakuwa kikwazo kikubwa katika maendeleo ya shughuli za kampuni hapa Zanzibar.

Kwa hivyo, kwa kuzingatia kasoro hizo na athari zake, wizara yangu imeona kwamba ipo haja ya kuipitia sheria hiyo na kuipendekeza sheria mpya ya makampuni.

Mhe. Mwenyekiti, madhumuni ya sheria hiyo ni kuwasilisha mapendekezo ya kutungwa sheria mpya ya kampuni itakayokidhi vigezo na mahitaji ya wakati huu ya kitaifa na kimataifa.

Vile vile shughuli hii itaweza kufanikisha shughuli za usajili na uendeshaji wa kampuni pamoja na shughuli za kibiashara kwa ujumla hapa Zanzibar.

1. Sheria hii inajaribu kuondoa vipengele vyote vilivyokuwemo kwenye sheria hiyo ya mwaka 2006 vilivyopitwa na wakati na vinavyokwaza shughuli za uendeshaji wa kampuni.

2. Sheria hii inaweka utaratibu mpya ambao utaendana na mabadiliko ya aina mbali mbali yakiwemo ya kiuchumi na kiteknolojia, ili kurahisisha uendeshaji wa shughuli za kampuni kulingana na mahitaji ya sasa ya kibiashara.

3. Inazingatia vigezo, utaratibu na mifumo ya kimataifa ya shughuli za uendeshaji wa makampuni.

Mhe. Mwenyekiti, faida zifuatazo zinatarajiwa kupatikana kutokana na kuanzishwa kwa sheria hii mpya tunayopendekeza:-

(i) Itapunguza vikwazo vya uendeshaji wa kampuni na kuondoa malalamiko kwa wafanyabiashara pamoja na wawekezaji kutokana na sheria iliopo sasa kupitwa na wakati.

(ii) Itaongeza muamko kwa wawekezaji wa ndani na nje, ili wawekeze Zanzibar kwa lengo la kuleta ushindani wa kibiashara.

(iii) Itarahisisha mfumo wa usajili wa biashara na upatikanaji wa taarifa zinazohusu bila ya usumbufu.

(iv) Itaongeza uwajibikaji na mashirikiano baina ya Afisi ya Usajili wa Kampuni, Taasisi za Leseni, Taasisi za Mapato, Wawekezaji pamoja na Kampuni kutokana na masharti mapya yanayowekwa katika sheria hiyo mpya.

(v) Kutaongezeka kwa idadi ya kampuni na kupunguza migogoro; kwa sababu sheria hiyo inatoa fursa kwa mtu mmoja kuunda na kumiliki kampuni.

Mhe. Mwenyekiti, katika mapendekezo haya na mswada huu unaanzishwa utaratibu wa usajili wa kampuni inayomilikiwa na mtu mmoja, ambao kwenye sheria ya sasa haupo.

(a) Utapunguza migogoro itokanayo na umiliki wa pamoja na kuongeza uwekezaji Zanzibar. Kwa mfano, sheria ya Tanzania Bara, Afrika ya Kusini, Marekani na Uingereza zimeweka utaratibu kama huo.

(b) Sheria hii mpya inaondoa msingi wa *ultravious*, yaani msingi huu ambao umo kwenye sheria ya sasa, unaweka mipaka ya uwezo wa Wakurugenzi kisheria, ili

kuwalinda wenye hisa, wawekezaji, wadeni wa kampuni na jamii kwa ujumla kwa kuhakikisha kuwa kampuni zinafanya kazi kwa mujibu wa malengo yake.

Hata hivyo, uhuru huo unaleta usumbufu katika uendeshaji wa kampuni, kwani umewezesha mtu mmoja ndani au nje ya kampuni kuishtaki kampuni mahakamani iwapo anahisi imekiuka Katiba na Kanuni ya Kampuni hizo. Jambo hilo linapelekea kampuni kuweka mlolongo mrefu wa malengo kwa ajili ya kuongeza wigo wa kazi, ili kuepuka kushtakiwa. Kwa mfano, Uingereza na Tanzania Bara zimeondoa misingi hiyo na sisi pia tunapendekeza hivyo kuondoa.

(c) Kwa kuwa inaondoa dhana hiyo niliyoisema hapo juu, basi rasmi hii inaweka misingi madhubuti ya kuwazuia Wakurugenzi wasitumie vibaya madaraka yao, ili kuhakikisha wanazingatia sheria, kanuni na maadili katika uendeshaji wa kampuni. Kwa mfano, kama kuanzia kifungu cha 185 na 186 ndivyo vinavyoeleza hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala la maslahi binafsi kifungu 187 na pia kufanya kazi kitaaluma kama kifungu 188 kinavyoelezea na hawaruhusu mgongano wa kimaslahi katika shughuli za kampuni.

(d) Sheria hii inalinda maslahi ya wenye hisa na wadau kwa kuwa inaweka masharti kwa wenye hisa watumie haki zao ikiwemo haki ya kushiriki vikao vya maamuzi kwa kuondoa haki ya kutumia uwakilishi.

Vile vile inaweka muongozo kwa wenye hisa wote wakubwa na wadogo, ili waweze kuwa na haki zinazowiana. Pia inaweka nafasi kwa wadau wakiwemo wafanyakazi pamoja na vyama vinavyowakilisha

kuwasilisha malalamiko yao dhidi ya matendo ya kampuni yanayokiuka sheria.

(e) Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo limezingatiwa katika mswada huu ni kwamba inaweka utaratibu wa kuwepo Daftari la Taarifa za Mikopo katika afisi za kampuni, ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa hizo kwa wadai pamoja na umma kwa ujumla inapohitajika. Sheria ya hivi sasa haielekezi utaratibu huu mpya.

(f) Katika mswada huu suala jengine ni kwamba inaweka utaratibu wa kupunguza hisa za kampuni na kuwalinda wageni nje ya utaratibu wa mahakama kwa kuutangazia umma na kuwaarifu wadeni nia ya kufanya hivyo. Kwa hivyo, wale wasioridhika wanaweza kupinga mahakamani kama vifungu vya 74 mpaka 77 vinavyoelezea.

Kwa utaratibu huo mahakama itakuwa na kazi ya kushughulikia maombi ya kupinga nia ya kampuni tu, na sheria ya sasa hairuhusu utaratibu huo na wala hairuhusu kupunguza mtaji wake isipokuwa kwa amri ya mahakama.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile katika mswada huu imeweka mfumo utakaoendana na vigezo vya usajili vya kimataifa ambavyo ni pamoja na kuzingatia uwazi, kufuata sheria za ndani za nchi na kuhakikisha kwamba mgawanyo wa madaraka miongoni mwa vyombo vya kusimamia na kutekeleza sheria hii umewekwa vizuri.

(2) Inahakikisha kwamba taarifa muhimu zinazohusu kampuni kama vile taarifa za fedha, umiliki na uwendeshaji wa kampuni zinatolewa kwa wakati na kwa usawa.

3) Wajumbe wa bodi za kampuni wanawajibika kwa kampuni na wanahisa, wanatenda haki kwa wadai wote na wanazingatia sheria, kanuni, maadili na maslahi ya kampuni.

4) Inaunganisha vifungu vya adhabu zitakazotolewa na mahakama iwapo mtu yeyote atakwenda kinyume na masharti ya sheria hii. Sheria ya sasa ina vifungu 36 vya adhabu. Idadi hiyo ni kubwa sana kwa vigezo vya kimataifa. Rasimu ya sheria mpya imepunguza vifungu hivyo vya adhabu.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kwa taarifa yako na kwa taarifa ya Baraza hili Tukufu niseme katika kutengeneza rasimu ya sheria hii, kumefanywa warsha mbali mbali zilizoandaliwa kwa lengo la kukusanya maoni na kupokea mapendekezo. Pia warsha hizo ziliwashirikisha wadau kutoka taasisi mbali mbali za serikali na za sekta binafsi zikiwemo taasisi za fedha, leseni, kodi, jumuiya za biashara, wafanyabiashara na wanasheria.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla muundo wa sheria hii ni kwamba una jumla ya sehemu 11, sehemu hizi zina vifungu 279.

Sehemu ya Kwanza: Inahusu utangulizi yenye vifungu viwili vinavyojieleza jina la sheria na muda wa kuanza kutumika pamoja na ufafanuzi wa baadhi ya maneno.

Sehemu ya Pili:Uanzishwaji wa Kampuni kutoka kifungu cha 3 mpaka kifungu cha 34. Vifungu hivyo vinaelezea utambuzi wa kampuni, vigezo vya usajili, katiba ya kampuni, jina linasajiliwa na wanamiliki wa kampuni.

Sehemu ya Tatu:Inahusu uwezo wa kampuni kutoka kifungu 35 - 44, vifungu hivyo vinaelezea mikataba ya kampuni, nyaraka za kampuni na muhuri wa kampuni.

Sehemu ya Nne:Inahusu hisa za kampuni na stakabadhi za mikopo ambayo ni kutoka kifungu 45 - 99, vifungu hivyo

vinahusu masharti mbali mbali kuhusiana na hisa na hati za mikopo.

Sehemu ya Tano:Inahusu usajili wa hati za mikopo kutoka kifungu cha 100 - 111, vifungu hivyo vinaelezea majukumu ya kampuni pamoja na rehani.

Sehemu ya Sita:Inahusu uongozi na uendeshaji wa Kampuni kutoka kifungu cha 112 -223 na vinazungumzia usajili wa umiliki, marejesho ya mwaka, mikutano, ukaguzi wa hesabu, wakurugenzi na maafisa wa kampuni na taratibu za mikopo.

Sehemu ya Saba:Inahusu wamiliki, kufunga kampuni kwa hiari na hii ni kutoka kifungu cha 224 – 237. Vifungu hivyo vinazungumzia mazingira yanayoweza kuifanya kampuni ifungwe kwa hiari pamoja na taratibu za ufungaji huo.

Sehemu ya Nane:Inahusu Kampuni zilizosajiliwa nje ya Zanzibar kutoka kifungu cha 238 - 254.Vifungu hivyo vinaelezea masharti ya kampuni za kigeni zinazoanzisha biashara Zanzibar na utangazaji wa hisa kwa kampuni za ndani na nje ya Zanzibar.

Sehemu ya Tisa:Inahusu masharti ya usajili ambayo inatoka kifungu cha 255 -258. Vifungu hivyo vinaelezea kuhusu ofisi ya usajili, ada za usajili, ukaguzi wa kampuni na utoaji taarifa kwa Mrajis.

Sehemu ya Kumi:Inahusu masharti juu ya biashara ya Benki na Bima na hii inazungumzia kutoka kifungu 255 - 262. Vifungu hivyo vinatoa maelezo kuhusiana na biashara za Benki na Bima, masharti ya ubia pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Sehemu ya Kumi na Moja:Inahusu masharti ya jumla na imeanzia kutoka kifungu 263 - 279.

Vifungu hivyo vinaelezea utunzaji wa vitabu na kumbukumbu za kampuni. Uwekaji na utoaji taarifa, makosa na adhabu zinazotokana na udanganyifu na kushindwa kutekeleza masharti mbali mbali ya sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kutokana na hayo naomba niwasilishe mswada huu ili Wajumbe waweze kuuchangia na kuwaomba watuidhinishie au waupitishe ili iweze kuwa sheria mpya ya makampuni. Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naomba kutoa hoja.

Mhe.Ussi Jecha Simai (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na afya njema iliyotuwezesha kukutana na kujadili Mswada huu muhimu wa kuifuta Sheria inayohusu Kampuni na Jumuiya Nyengine.

Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, nitangulie kusema kuwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi inaunga mkono uamuzi wa serikali kwa kuleta Mswada huu wa Sheria ya Kufuta na Kuandika Sheria Inayohusu Kampuni na Jumuiya Nyengine, Kuweka Masharti Madhubuti Zaidi ya Uratibu na Udhibiti wa Kampuni, Jumuiya na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo. Mbele ya Baraza lako tukufu kwa madhumuni ya kurekebisha sekta ya uwekezaji nchini ambayo imekuwa na changamoto nyingi hivi sasa, ambapo kwa namna moja ama nyengine sheria hii itakapoanza kutumika itasaidia kuzitatua baadhi ya changamoto hizo.

Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa mkosefu wa fadhila endapo sitowashukuru wadau ambao Kamati yetu ilikutana nao kuujadili mswada huu na kutupatia maoni yao ambayo kwa kiasi kikubwa yameisadia Kamati kutoa mapendekezo muhimu katika marekebisho tuliyoyatoa.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na kukua kwa sekta ya uwekezaji, ni wazi kuwa kuna haja kubwa ya kuzirekebisha sheria zetu na kuzifanya bora zaidi ambapo zitasaidia kuwaongoza wadau wa sekta hiyo na kurahisisha biashara na maisha ya wananchi walio wengi. Aidha kuimarika kwa sekta ya uwekezaji kutaongeza ari ya ushindani wa kibiashara miongoni mwa wafanyabiashara na kuimarika kwa pato la taifa kwa kiasi kikubwa na kuitangaza nchi yetu Kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa Mswada huu, vipengele vyote vilivyomo katika Sheria ya makampuni vilivyopitwa na wakati vimeondolewa na kumewekwa utaratibu mpya ambao utasaidia kurahisisha uwekezaji hapa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ilipitia Mswada wa Sheria ya Kufuta na kuandika Sheria inayohusu Makampuni na Jumuiya nyengine ambapo marekebisho mbali mbali yalifanywa na Kamati kwa umakini mkubwa. Naomba nichukue fursa hii kuwataja Wajumbe wa Kamati hiyo kama ifuatavyo:

1. Mhe. Ussi Jecha Simai - Mwenyekiti
2. Mhe. Abdalla Juma Abdalla - Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Bikame Yussuf Hamad -Mjumbe
4. Mhe. Salim Nassor Ali - Mjumbe
5. Mhe. Suleiman Hemed Khamis - Mjumbe
6. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Mjumbe
7. Ndg. Aziza Waziri Kheir -Katibu
8. Ndg. Khamis Hamad Haji - Katibu

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba uniruhusu nieleze baadhi ya marekebisho na mapendekezo ya Kamati yaliyofanywa na Kamati yetu, aidha naomba niwatanabahishe Waheshimiwa Wajumbe kuwa, hotuba hii inatoa ufafanuzi kwa baadhi tu ya vifungu ambavyo vimependekezwa kufanyiwa marekebisho na Kamati, hivyo maelezo zaidi ya mapendekezo hayo naomba muangalie katika muhtasari wa marekebisho yetu ambayo Waheshimiwa Wajumbe tayari mmeshapatiwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 3 cha Mswada huu kinachohusu Katiba ya ushirikiano na namna ya kuunda Kampuni iliyoandikishwa, Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Wizara ya kuongeza kijifungu kipya cha (2) ambacho kinasomeka

"Mtu yeyote anaweza kuunda kampuni ya dhima yenye ukomo itakayojulikana kama kampuni binafsi ya mjumbe mmoja kwa kuweka jina lake katika katiba ya kampuni, na kwa kutekeleza matakwa ya Sheria hii yanayohusu usajili"
Kutokana na umuhimu wa kifungu hiki Kamati imekubaliana na pendekezo la kuongeza kifungu hicho''.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu pia inapendekeza katika Sehemu ya Pili ya Mswada huu ambayo inatoa ufafanuzi wa tafsiri za maneno kuwa baadhi ya maneno maana zake haziko vizuri na zirekebishwe. Kwa mfano neno "Wakala" halileti maana sahihi ya nani wakala, hivyo litafsiriwe maana ya wakala na ieleze anapozungumziwa wakala anajumuishwa nani na nani. Kutoa maana sahihi ya neno hilo kutasaidia kujua wakala ni nani na ana wajibu gani katika kampuni na taasisi nyengine zilizozungumzwa katika mswada huu. Aidha katika sehemu hiyo ya tafsiri, Kamati ilitoa maelekezo ya kurekebishwa baadhi ya maneno hayo kama inavyojieleza katika Marekebisho yetu ambayo tumeyawasilisha kwako.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu katika kifungu cha 4 (1) (a) neno "*Limited*" lisomeke "Ukomo" au lianzie neno la Kiswahili kwanza baadae lifuatie hilo neno la Kiingereza ili kuwasaidia wananchi wetu kujua kilichokusudiwa kutokana na watumiaji wengi wa sheria hii kuwa ni wananchi ambao lugha wanayoifahamu kwa urahisi zaidi ni Kiswahili. Hivyo matumizi ya neno hilo yatatusaidia kufahamu kilichokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, Katika kifungu cha 5 Kamati ilipendekeza neno "Mwanasheria" liondoke na badala yake liwekwe neno "Wakili". Kamati ilipendekeza hivyo kutokana na uhalisia kuwa mwanasheria anaweza akawa hata mwanafunzi aliyemaliza chuo kwa wakati huo, hivyo jambo hilo linaweza likaleta matatizo kwa uwajibikaji wa huyo mwanasheria kutokana na ukweli kwamba kazi hizi zinahitaji uzoefu na uwajibikaji ulio makini, hivyo kumuweka mwanasheria ambaye hana uzoefu kutasababisha matatizo katika utekelezaji wa sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, Kifungu cha 19 (4) Kamati imependekeza neno "Shirika" liondoke na liwekwe neno "Taasisi". Kamati imependekeza hivyo kutokana na maana halisi ya neno Shirika na Taasisi kuwa na maana tofauti, na hivyo kuona umuhimu wa kuweka neno taasisi ili kuondoa tofauti ambazo zingejitokeza katika utekelezaji wa Sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati pia imependekeza katika kifungu cha 40 maneno "Hati" na "Nyaraka" yatolewe tafsiri yake katika sehemu ya Tafsiri na baada ya kutolewa tafsiri hiyo yatumike kwa mujibu wa hiyo tafsiri ili kuondoa utata uliopo hivi sasa ambapo maneno hayo katika mswada huu yametumika pasi na kuangalia tafsiri ya maneno hayo kiuhalisia.

Mhe. Mwenyekiti, Kifungu cha 42 cha Mswada huu katika maneno yake ya pembeni ambayo yanasomeka "utekelezaji wa hati" imependekezwa na Kamati kuwa maneno hayo yasomeke

“utiaji saini wa hati” kutokana na maudhui ya kifungu hicho yalivyo na utekelezaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati pia imependekeza katika kifungu cha 67 maneno ya pembeni neno “Viasi” liondoke na liwekwe neno “Hisa” kutokana na maudhui ya kifungu hicho yalivyo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati pia imefanya marekebisho katika kifungu cha 225 neno “Gazeti” liongezewe maneno “Rasmi la Serikali”.

Mhe. Mwenyekiti, Kifungu cha 259 kimerekebishwa na Kamati kwa kuliondoa neno “Chama” na kuweka neno “Taasisi” kutokana na maneno hayo mawili kuwa na maana tofauti, hivyo Kamati imeona ni vyema kutumia neno “Taasisi” ili kuifanya sheria hiyo itakapoanza utekelezaji wake kusiwe na mkanganyiko wa maneno.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa tunaiomba serikali kuyazingatia yale yote yaliyopendekezwa na Kamati na wadau wa taasisi mbali mbali ambao kwa namna moja au nyengine wamesaidia kutoa maoni yao ili kuifanya Sheria hii itakapoanza kutumika iwe ni bora zaidi. Kufanya hivyo ni kuisaidia serikali na taasisi husika kuepukana na adha na usumbufu uliokuwa unajitokeza wakati wawekezaji wanapojitokeza na kutaka kuwekeza hapa nchini.

Aidha Kamati inapenda kuishauri Wizara na serikali kwa ujumla kushirikiana na sekta binafsi kupitia makampuni ili kuimarisha sekta ya uwekezaji nchini ambayo ndio tegemeo kubwa la kukua kwa uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kueleza hayo, nawaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu, hekima iwatangulie na busara iwatawale ili wauchangie, waurekebishe Mswada huu kwa kutoa mawazo

yatakayosaidia katika kuufanya uwe bora zaidi, na hatimaye kuupitisha ili usaidie kuleta ufanisi katika nchi yetu.
Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa ni zamu ya wachangiaji, mpaka sasa bado sijapokea jina la mtu hata mmoja na majadiliano yanaendelea. Waheshimiwa Wajumbe wale ambao wapo nje tungeliwaomba waingie ndani ili tuweze kuja kufanya kazi tuliyotumwa na wananchi. Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea.

Mhe. Abdalla Moh'd Ali: Mhe. Mwenyekiti, Nashukuru asubuhi hii kunipatia fursa ya kuzungumza machache kuhusu Mswada huu. Matumaini yangu Mhe. Mwenyekiti, kuja kwa Mswada huu kutapunguza *longolongo* zilizopo katika uendelezaji wa shughuli za uchumi katika nchi hii. Nawashukuru sana watu wa Kamati kwamba wameona mengi na wamependekeza mengi, sisi wengine tumepata kidogo tu. Nina imani nayo yataongeza ufanisi wa Mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitokuwa na mengi isipokuwa kuna kifungu kidogo kimoja tu ambacho nahisi na mimi ningetoa maoni yangu. Kifungu hichi ni kifungu cha 20 ambacho kinasema:-

"Kama Mrajis ataona kwamba jina ambalo kampuni imesajiliwa linapotosha maumbile ya shughuli zake, na kama kuna uwezekano wa kusababisha madhara kwa umma anaweza kuelekeza kubadilisha jina lake".

Mhe. Mwenyekiti, mimi labda ningemuomba Mhe. Waziri akanipa maelekezo kidogo, kwa sababu hapa kuna mambo mawili. Ataona kwamba kuna jina la Kampuni lilisajiliwa linapotoshwa, hili ni suala la kwanza. Suala jengine kwamba kutakuwa kuna umma unapotoka. Kwanza ningeanzia huko kwamba labda umma utakuwa unapotoka au kutakuwa kuna

madhara kwa umma. Sijui ni kigezo gani ambacho kama Mrajis atakitumia katika kuona kwamba hivi sasa jina hili linaweza kuleta athari kwa umma.

Ninachokifahamu mimi kwamba si rahisi kwamba asilimia zote 100 kwamba zikubaliane na fikra fulani. Isipokuwa kila mmoja katika mtazamo wa kitu inawezekana akawa na imani yake. Sasa labda wao katika kupima hilo watatumia kigezo gani katika kujua kwamba hapa sasa huu umma umeanza kupata madhara kwa sababu ya kutumia jina hili au kwa sababu ya kutumia jina hili. Wengine labda katika uletaji wa majina huwa wana lengo fulani au labda pengine kampuni yake inawezekana akawa kalenga watu wa aina fulani tu sio umma kwa ujumla.

Kwa maana hiyo kuweka jina lile kutawafanya wale watu waje kwa haraka kwa sababu ya upenzi wa lile jambo liliopo, labda kwa hivi sasa tunaweza tukasema kwamba mimi naweka jina langu labda Usama Bin Laden kwa sababu fulani labda kwa wale wanaokwenda Makka wanajua kuwa Usama Bin Laden ndiye anayehudumia misikiti ile miwili ya Makka na Madina. Sasa kufanya vile pengine kutavutia wale watu ambao wanataka kwenda, lakini pengine jina hili katika umma kiujumla labda wengine hawalipendi kutokana labda na zile tabia za mtu huyu kwa baadhi ya watu. Sasa labda ningelipenda Waziri akanifahamisha kwamba watatumia vigezo gani kujua kwamba hapa sasa umma utaathirika kwa kuwepo kwa jina hili.

Mhe. Mwenyekiti, labda niende kwenye jina. Kumependekezwa kwamba labda kifungu cha 4 cha Mswada wa Kiingereza umesema kwamba *"Shall be printed in English or Kiswahili"* mimi naona labda tungeweka tu kwamba *"Shall be printed in Kiswahili and English* isiwe *or* ikawa inapatikana moja, bora ingelikuwepo katika lugha zote mbili kwa ulinganisho. Kwa sababu mimi pengine naweza nikaipata ya Kiswahili nikaisoma ya Kiswahili, na mwengine akawa ana wa Kiingereza akapata ulinganisho kama inavyokuja miswada yetu mengine hapa

Barazani. Sasa ili kuiandika kwa lugha moja tu naona itaondoa upeo wa kusoma, kwa sababu wengine wanaweza wakataka *exemplary* yaani *demonstration* pengine kwa lugha ya Kiswahili wakajua wakopie vipi kwa wale ambao pengine wanataka kuandika kwa lugha ya Kiingereza. Kuna wengine wanaweza wakafanya *thesis* zao kwa kutumia mambo kama haya au sheria kama hizi au kampuni kama hizi zinapokuwepo. Sasa ile *access* ya labda wale wanaotakakufanya *thesis* ambao wao pengine lugha zao ni Kiingereza, basi wakapata kwa ile mifano ambayo ya kampuni zilizopo Zanzibar zilizokuwa hazijasajiliwa za nje.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia hapa kuwepo tukiwa wazima na afya njema, lakini pia nikushukuru wewe Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niwe miongoni mwa wachangiaji wa Mswada huu kutokana na kuwa na sekta hii ya uwekezaji ni muhimu sana kwa Taifa letu, basi ni wazi ipo haja ya kuzifanyia marekebisho sheria zetu hizi na kuzifanya ziwe bora zaidi kwa maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, naamini kwamba Kamati ya Katiba na Sheria imeupitia Mswada huu kwa umakini mkubwa na kwa uwezo mkubwa walionao na kufanya marekebisho mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitokuwa na mengi sana, lakini niseme kupita kwa sheria hii na kama serikali tutaifanyia kazi ipasavyo sheria hii, basi naamini kwamba nchi yetu kwa kweli itapiga hatua kubwa ya kujikwamua na umasikini, lakini pia kuendelea nchi yetu katika uchumi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, naamini kwamba kama nilivyosema awali sitokuwa na mengi, lakini nimesimama hapa ili kuupongeza Mswada huu lakini pia kuunga mkono na kumuomba Mhe. Waziri kwamba Mswada huu ni mzuri, lakini nirejee kusema kwamba tusiuweke tu kwenye makabati, basi ni vyema tuufanyie kazi kwa maslahi ya nchi yetu.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, nauunga mkono Mswada huu mia juu ya mia. Nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa Mjumbe, majadiliano yanaendelea. Waheshimiwa Wajumbe Majadiliano yanaendelea, majadiliano yanaendelea. Nafikiria si jambo la busara kumuita Mhe. Waziri kuja kufanya majumuisho kwenye hili, wakati sote tupo hapa kwa ajili ya kazi hii. Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii ya kuchangia mswada huu. Mswada huu ni mzuri sana na niseme baada ya kuupitisha mswada huu tutaona mafanikio yatakayojitokeza, kwani kuna mabadiliko mengi katika mswada huu, si rahisi kwamba tutauchangia kwa uchache kwa sababu una vifungu vingi na ni muhimu sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa kuwasilisha mswada wake huu na vile vile niipongeze Kamati kwa kutoa maoni yake mbali mbali kuhusiana na Mswada huu. Kama tunavyojua kwamba Sheria hii ni sheria ambayo ni ya muda mrefu tokea mwaka 1948 iliyoletwa na Waingereza. Kuna nchi ambazo zimetawaliwa na Waingereza basi bado wanatumia sheria hii, lakini siku zote sheria ni lazima zifanyiwe mapitio kwa sababu kuna baadhi ya vifungu vinakuwa vimepitwa na wakati.

Mhe. Mwenyekiti, tulipopata Semina ya Mswada huu imeonesha kwamba Zanzibar ni nchi ambayo mpaka sasa hivi ukitizama

katika *status* ya biashara; vile viashiria vya biashara katika dunia ni kwamba Zanzibar kwa mwaka kama sikosei 2012 kwamba nafasi yetu ilikuwa 155 na kwa *East Africa* tulikuwa ni watu wa 6 na ikawa ni watu wa mwisho. Lakini vilevile ni kwamba sheria hii ili tuweze sasa kujiweka katika nafasi na sisi kama Zanzibar tukawa tunaenda kwa mnasaba wa sheria hii kwamba tukawa tunaenda na wakati na zile sheria za ulimwengu ili sasa tuone ni nafasi gani ambayo tutachukua kutokana na kuona sheria hizi zimekuwa za muda mrefu na zimeshapitwa na wakati.

Mhe. Mwenyekiti niulize suali moja tu kwenye hii *company liability* ambayo kwamba kama utakuwa na mtaji wako wa shilingi milioni moja, ukiweka milioni moja basi itakuwa ni *company liability* kama utafilisika kwa kuwa na madeni, milioni 300 basi hata uwe na majumba, magari, mashamba kitakachochukuliwa ni *company liability* ya milioni moja. Sasa nimuulize Mhe. Waziri hili deni jengine kama pengine la shilingi milioni mia tatu lakini kwa sababu *company liability* ni shilingi milioni moja hizi nyengine milioni mia mbili atalipa nani au itakuwaje kuhusu hili deni la shilingi milioni mbili lililobakia?

Mhe. Mwenyekiti kwa kweli mswada huu ni muhimu na madhumuni yake ni mazuri. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti kama nilivyokuwa ninasema mara nyingi kwenye Baraza hili kuja wanasheria, na mimi kwa bahati mbaya si mwanasheria, kwa hivyo niwaambie wenzangu katika Baraza lako hili huu mswada tuupitie, tuukosoe na baadae tuupitishe kwa mafanikio ya nchi yetu hii ya Zanzibar.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nasema naunga mkono mswada huu mia kwa mia. Ninakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa fursa hii.

Mhe. Farida Amour Mohamed: Ahsante Mhe. Mwenyekiti nami kunipa nafasi ya kuchangia mswada huu japo maeneo mawili matatu. Kwanza naomba pia nimpongeze Mhe. Waziri

jinsi alivyowasilisha mswada wake huu muhimu katika wakati huu tulionao.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme sheria hii ingeliweka utaratibu wa kukagua maendeleo zile kampuni zilizokuwa tayari zishasajiliwa. Maana mbali ya zile tayari za usajili lakini na zile kampuni zilizokuwa zimeshasajiliwa angalau ziwe na utaratibu maalum wa kukaguliwa. Mtazamo wangu Mhe. Mwenyekiti si hoja ya kusajili tu lakini na faida ile itakayopatikana katika nchi yetu baada ya kusajiliwa zile kampuni. Kwa sababu kuna kampuni nyingi zishasajiliwa kubwa na ndogo za nje na za ndani, sasa zaidi tungelitilia mkazo hizi kampuni zetu za ndani ndogo ili kupata yale maslahi na maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti hofu yangu ni kuwepo kwa daftari lenye kusheheni kampuni nyingi lakini faida zake zikawa hazionekani. Sasa katika hili namuomba Mhe. Waziri awe na utaratibu maalumu wa kukagua kampuni tayari zilizokuwa zimeshasajiliwa.

Mhe. Mwenyekiti jambo jengine muhimu ni kuwepo utaratibu wa kuziwezesha na kuzisaidia kampuni zilizokuwa tayari zishasajiliwa, hasa kampuni za ndani na zinazosimamiwa na akinamama. Kwani kuwasaidia kinamama katika kampuni hizi ndogo ndogo ni kuisaidia nchi, kwani Mhe. Rais anatangaza sana kuhusu suala la kujiajiri wenyewe, sasa wakati kuna wanawake kinamama washajikusanya wenyewe kujisajili kwa kampuni zao ili kupata kuwasaidia.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 92 (c) ukurasa wa 186 kuna lugha inahitaji marekebisho kwa maoni yangu. Kifungu hiki kimeandikwa anakuwa na akili isiyokuwa timamu. Sasa nashauri kiwe anakuwa na ugonjwa wa akili yaani kisomeke cheo cha Mkurugenzi kitakuwa wazi iwapo Mkurugenzi ana ugonjwa wa akili, hapo itafahamika zaidi kuliko vile ilivyokuwa mwanzo.

Mhe. Mwenyekiti kifungu namba 5 ukurasa wa 22 kimeandikwa, Katiba itathibitishwa na Mwanasheria anayefanya kazi za kisheria, lakini haikufafanua kufanya kazi za kisheria wapi na taasisi ipi. Sasa nadhani hilo pia ni muhimu kufanyiwa utafiti ili likafafanuka zaidi.

Na kifungu cha 26 ukurasa wa 30 kinasomeka Kampuni itapeleka kwa mwanachama itapotakiwa nakala ya Katiba na Kanuni *kama zipo*. Mhe. Mwenyekiti, hili neno *kama zipo* kiukweli kinafanya hiki chote kiwe hakileti maana nzuri. Kwa sababu kama maneno haya yakiendelea kuwepo siku zote kuwa Wakurugenzi wa Kampuni watasema Katiba na Kanuni hazipo itakuwa kiukweli hapako sahihi. Kwa hivyo naomba hapa pawe na mabadiliko ili watu wetu wapate fursa; wanachama wa kampuni kupata Katiba na Kanuni za Kampuni. Nashauri *kama zipo* yaondoke lirekebishwe vyengine.

Mwisho Mhe. Mwenyekiti naunga mkono hoja hii ya Waziri lakini tu namuomba Mhe. Waziri aandae utaratibu wa taaluma kwa wananchi. Kwa sababu jambo lolote lile ikiwa huna taaluma inakuwa hupati kufanikiwa, kwa hivyo paandaliwe utaratibu maalumu wa kuwapa taaluma wananchi wote wa Zanzibar ili wapate kuufahamu zaidi huu mswada. Naunga mkono hoja. Ahsante.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kuweza kupata fursa hii ya kuweza kuchangia mswada huu wa sheria ya kufuta na kuandika sheria inayohusika na Kampuni za Jumuiya nyengine na kuweka masharti madhubuti ya utaratibu wake. Mheshimiwa mimi nimefurahi sana kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri na Katibu wake na watendaji wake kutokana na hali halisi ambayo kuna mambo ambayo kwenye makampuni yanakuwa yana kasoro, na leo kuweza kuletwa hapa ili kuweza kufanya marekebisho ambayo yatakuwa sahihi kwa mujibu wa sheria ya Baraza letu hili na kuweza kupitisha kwa vizuri kabisa.

Mhe. Mwenyekiti mimi nakubaliana nalo na kitu ambacho ninachokubaliana nacho mara nyingi sana Mhe. Mwenyekiti mimi sina hoja kubwa, kwa sababu kitu kizuri ambacho kinachotaka kuletwa hapa na hasa wananchi wetu wengi wanafahamu vyengine sana utafauti wa kufungua kampuni wanakuwa wanaona ni lazima kampuni ina watu *special*, ambao wanaoruhusika kuweza kufungua makampuni hayo hilo wanalifahamu, na ndio maana wakawa woga kabisa katika ufunguaji huo. Lakini leo sheria hii inatuonesha hasa kuwa mtu yeyote kwa mujbu wa sheria na masharti yaliyowekwa kwenye Wizara hii au kwenye kitengo hiki cha usajili cha Mrajis mwenyewe, basi anaruhusika kuweza kufungua kampuni kwa mujibu wa taratibu mimi sina tatizo nalo, tena nakubaliana nalo mia kwa mia.

Lakini ningeomba kwanza Wizara wangejaribu kufanya semina kwa kupitia wananchi katika sheria zetu ili kuweza kuwaelimisha hasara na faida za kuwa na kampuni. Hili ni moja ambalo nimegundua hawana elimu hiyo ni watu wachache sana na utakuta ni wengi ambao wananufaika kwenye makampuni ni watu wachache sana.

La pili ambalo nataka nitahadharishe zaidi kabda sijaendelea kwenye vifungu zaidi Mhe. Waziri atanisaidia, kuna watu ambao huwa wajanja wanasema kuwa tayari kampuni keshafungua anakwenda kuomba kitu kwenye ardhi na kuonesha *document* ambayo tayari, kumbe hajafanya usajili huo. Sasa sijui Mheshimiwa watu kama hawa kwa mujibu wa sheria, unajua leo sikuvaa miwani Mhe. Mwenyekiti, sijui hukumu yake ikoje. Nataka nione lakini nafikiri Mhe. Waziri atanisaidia kwa sababu si mchoyo, na yeye kuweza kumuelimisha mtu sheria. Kwa sababu sijaona hukumu yake ikoje mtu kama huyo kwa sababu mambo kama haya yanapoteza mapato sana katika serikali na ni udanganyifu mkubwa sana hasa katika nchi zetu, kwa sababu unapofanya hapa hili suala lako linaendelea katika Umoja wa

Mataifa. Mimi nafikiria Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ningeomba sana hili suala kama sheria humu humu ya kumdhibiti mtu kama huyo imo kwa sababu hili suala kubwa sana, huu msahafu wake mkubwa huu. Kwa hivyo ningeomba sana kuwa sheria hiyo ipatikane kuweza kumdhibiti.

Lakini naendelea Mheshimiwa katika ukurasa huu wa 22 hapa kwenye ushirikiano wa kanuni zinazoeleza taratibu. Mheshimiwa kwanza mimi nikubaliane nazo katika kifungu hiki cha 8 kama kinavyoeleza inawezekana kuwa kampuni yoyote kuwa ukomo wa hisa au kwa kampuni yoyote ukomo wa dhamana isiyokuwa na ukomo wasajiliwe ili Katiba na Kanuni na zishirikishwe kuwachangia kwenye katiba ambayo taratibu zinazowekwa kwa Kampuni, mimi nakubaliana nazo. Na wengi sana Mheshimiwa nimegundua wengine wanakuwa hawana kanuni, hasa kama mtu anakusudia kutaka kufanya ubadhirifu hawana kanuni au zile sheria ndogo ndogo, hawaoneshi jinsi gani ambavyo na nani, Mheshimiwa watu wengi sana wameshaibiwa kusema la ukweli.

Nataka niwatahadharishe hasa ndugu zangu za kizanzibari ambao wawekezaji wengi sasa hivi wanakuja hapa, na wakija wanawachukua Wazanzibari kuwashirikisha katika kuwafungulia kampuni na akamtangazia akamwambia nakupa hisa kubwa, lakini leo hisa ile Mhe. Mwenyekiti inakuwa ni vichekesho vikubwa sana, wanapokuwa wanagombana anadai hisa ile lakini utagundua sheria haimpi ile hisa aipate kwa sababu kuna mchezo umechezeka pale, ambao kwa mujibu wa sheria na ndio maana nikasema kuwa sheria hizi za makampuni ninamwambia Mhe. Waziri na Mrajis wazishushe chini ili wananchi wanufaike, wanaingia mtego mkubwa sana Mheshimiwa wanapoteza mambo yao chungu nzima, wanapoteza mali zao na watu ni wanyonge Mhe. Mwenyekiti ni wanyonge kabisa.

Inasikitisha sana, sasa naomba sana Mheshimiwa mimi nakubaliana nacho kifungu hicho wala sina tatizo nacho, kwa

sababu ni lazima ieleweke zile hisa zenyewe kwa mujibu wa kanuni na katiba zao ili mshiriki afahamu, lakini sasa nitauliza atafahamu vipi wakati hajui sheria, je tunaruhusika kuwa mtu kama yule kwanza kabla ya kusaini ile akamchukue Mwanasheria wake, lakini atampata vipi mwanasheria wake wakati yeye yule hajui kama utaratibu ule, yeye anakimbilia tu kwamba mwaka huu mimi nitatajirika tu madhali mzungu kama hapa na nini. Hili ni suala ambalo Mheshimiwa kwa kweli haileti mantiki vizuri wala halitosaidia katika uendeshaji wa mambo kama hayo.

Mheshimiwa nikiingia katika ukurasa wa 25 hasa hapa nafurahi sana kuonesha kuwa kanuni zenyewe nimeziainisha hapa zimechapishwa kwa lugha ya Kiingereza au kwa lugha ya Kiswahili, zimegaiwa katika *paragraph* zenye nambari za kufufuliza zimeshuhudiwa na Mwanasheria na kutiwa saini na kila mchangiaji kwenye katiba ya ushirikiano huo.

Mhe. Mwenyekiti niseme kuwa *almost* watu wa Zanzibar wanazungumza lugha ya Kiswahili hii tukitaka tusitake, na hapa mara nyingi sana tunapigwa changa la macho tusojua Kiingereza, hii ukweli tuseme si aibu mimi kusema sijui Kiingereza wakati mimi lugha yangu ni Kiswahili. Najinasibu sana kusema Kiswahili ndani ya Zanzibar kwa sababu ni lugha yangu kabisa ki-*international* haina tatizo mimi hilo. Lakini na wajanja hapa ndio wanapotumia njia zao nakubali mimi *system* hiyo kuwa *paragraph* ya mwanzo lugha ya Kiswahili, au *paragraph* lugha ya Kiingereza *and then* ije lugha ya kizungu *that is ok* mimi sina tatizo nalo Mhe. Mwenyekiti hata kidogo.

Sasa mara nyingi sana mimi hupiga kelele hata kwenye mikataba ya kazi wananyang'anywa wananchi kwa misingi hii hii, lugha kubwa hii ya Kiingereza si mchezo, si wengi sana wanaojua Kiingereza bwana. Lakini utakuta ndio wengi sana wanafanya mchezo kama huo, hii mimi namshukuru sana Mhe. Abubakar kaiona hii Mhe. Waziri hili suala nakuunga mkono kabisa kuwa

hapa pakazanieni kifungu hiki Mhe. Mrajis, *otherwise* tutawadhalilisha wananchi wetu kutokana na lugha iliyokuwa ngeni na wao, tuwe *serious* hii nakubaliana nayo kabisa. Nakubaliana nalo suala hili kuwa *okay* tuwe na lugha hiyo hata kama Kiitaliana, lakini lazima *translation* yake ya Kiswahili kiwepo. Mheshimiwa hizi kanuni nimefurahika nazo kusema la ukweli kuwa umetumia hapa, sasa kweli unataka kuwasaidia Wazanzibari na kuweza kusaidia ili kuweza kupata utajiri wao.

Mheshimiwa niende katika hizi taaluma ya kuzingatia sheria ya masharti yaliyomo katika makampuni inayosema kwa azimio maalumu kubadilisha au kuongeza vifungu kwenye kanuni zake. Mheshimiwa siku hizi kuna taratibu watu wajanja, anaweza mtu akafanya ujanja wa kubadilisha badilisha bila ya wewe mshirika huna taarifa hiyo. Sasa hii nayo kuona hapa imeingizwa nakubaliana nayo, fomu ambayo Katiba ya Ushirikiano ya Kampuni yenye ukomo ya hisa, katiba na kanuni za ushirikiano za kampuni yenye ukomo na dhamana isiyokuwa na mtaji wa hisa, Katiba na Kanuni za ushirikiano yenye ukomo na dhamana mtaji wa hisa na Katiba ya Kanuni ya ushirikiano ya Kampuni isiyo na ukomo yenye mtaji katika hisa zitakazokuwa na fomu ambazo zenye majaduweli A, B, C, D, E, na F.

Mhe. Mwenyekiti nawapa hongera sana na mara nyingi sana husema saa nyengine Dr. Shein huchagua viongozi ambao wenye kuona na wenye kufahamu, sasa hivi ndio tunavyopenda jamani kuwa sheria zisikae muda mwingi ziwe zina mabadiliko kutokana na wakati, kwa sababu wakati wa nyuma na wa leo tofauti, sheria leo zina upana mwingi na halafu kwenye sheria kila ukimuweka kijana ndio anazidi kuona sheria. Sasa mimi nakubaliana nalo hili mimi sijapata kuona fomu za aina kama hii Mhe. Mwenyekiti kutolewa, ndio kwanza nione *system* hii mpya, ama kweli kila jambo ambalo lenye kutaka kuongoza sheria iweke sawa basi ndio hii, mimi nakubaliana na fomu hizi sina *objection* hata kidogo, lakini usimamizi wake Mhe. Waziri naomba sana uwe na usimamizi mzuri katika fomu hizi naomba

kabisa. Bei zao zisiwe za ukomo za kushindwa kuja kuchukua fomu tukaendelea na ukiritimba ule ule ambao tunaoukataa, kwa sababu inawezekana fomu mkatoa ikawa bei yake zikawa ziko juu, hatimaye ndio yale yale tumeunda sheria na tumerudi hapa hapa.

Mhe. Mwenyekiti, nikishuka chini hapa nasema isipokuwa Waziri anaweza katika kipindi tofauti cha kurekebisha jaduweli yote kati ya hizo katiba na kanuni kama zipo zitawasilishwa na Mrajis ambaye atazisajili na kubaki nazo. Ndivyo inavyotakiwa hivyo, lazima Waziri aone hilo na kama kuna jambo kaliona lina *mistake* anaweza sheria hiyo kuibadilisha ili kuweza kusaidia hali halisi ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti haya makampuni yetu Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo mengine niseme labda *power* mnapokuwa mnawafanyia *registration* kwa lengo la kutaka kuleta neema ya kuweza kumsaidia kwa wingi acha *members*, hata na wale watu watakaopata, kwa sababu kampuni nyengine zinafanya hapa kwa makusudi kwa mfano kujenga Bandari, kujenga mambo mengine ya nyumba ya mkopo nafuu na mambo mengine mengine, kujenga ustawi wa michezo na nashukuru sana habari ya michezo kuwa Mhe. Waziri amekubali sasa hivi wanariadha karibu watafanya uchaguzi wao, nimshukuru kwa hilo na *inshaallah* Mungu ambariki na uchaguzi wetu kwa salama kabisa.

Mheshimiwa kuna mambo ambayo yanatakiwa yafanyiwe haraka sana hizi kampuni zinakuwa zinalalamika kuna mambo mengine wanakosa kufanyiwa haraka, ushafanyiwa usajili kwa mujibu wa sheria, ushakuwa unatambulikana sasa hivi katika *government* kwa mujibu wa utaratibu ushapewa *certificate* pale sasa kuna fursa ambazo zinatakiwa azipate ndani ya ile serikali yenyewe, Mheshimiwa kuna *delay* hapo ndipo tunapokuwa tunawavunja moyo wale watu wa makampuni. Nalo hili naomba sana Mhe. Waziri kama limo humu kwa kuwa miwani sina

nakuomba sana nalo hili lichukuliwe na uweze kulifuatilia kwa sababu kuna mambo ambayo kusema kweli Mheshimiwa mpaka leo makampuni mengine yanadhalilishwa wanatafuta ardhi za kuweza kufanya mambo yao lakini bado wanahangaishwa huku wanafanyia hivi, mwisho wanafika pahali wanatapeliwa. Mheshimiwa nina uchungu kabisa watu wengi sana wameshatapeliwa makampuni haya halafu wanapita wakasema huko nje, tumeshafanya *registration* tumelipa ada inavyotakiwa tunakaguliwa kila baada ya mwaka halafu leo hatusimamiwi.

Mheshimiwa kwa kweli huwa naona uchungu sana kuwa leo kitengo kinachohusika hakitusimamii tukapata haki zetu, sasa sijui kuwa wale hawajui kuja kulalamika kwenu, hakuna utaratibu huo, kwa hivyo kama hakuna utaratibu huo naomba *the first time* mnapowapa *certificate* basi muwaelimishe, and *then* ili wasiweze kupata matatizo na kurudi kwao. Mheshimiwa hilo ni suala ambalo kwa kweli mimi linanisikitisha sana, tayari makampuni mengi huko nje yanatusema vibaya sana Mhe. Mwenyekiti. Tunawafungulia sheria tunawaambia njooni muwekeze, lakini kuwekeza kwenu kwa mujibu wa sheria nataka mufanye *registration* katika Zanzibar kwa mfumo wa kampuni, haya matatizo Mhe. Mwenyekiti hili suala wanafanya. Lakini kinyume chake ukanda ule wa kwangu kwa mfano kule Kiwengwa, mambo mengi sana kwa kweli watu hawakufaidika vizuri sana katika mfumo huo. Naomba sana Mhe. Waziri hili suala uweze kulisimamia kwa uangalifu kabisa.

Mheshimiwa ukurasa wa 26 masharti yaliyohusika kubadilisha na kampuni. Mabadiliko ya jina hapa nimegundua ujanja mkubwa sana Mheshimiwa nataka nikufunue macho leo Mhe. Waziri, mimi siku zote kawaida yangu Mheshimiwa mara hii tu nimekosa kwenda Makka lakini *inshaallah* Mwenyezi Mungu akinijaalia mara nyengine nitakwenda Makka. Sasa kusema ukweli ndio unapata fursa ya kwenda Makka, na kwenda kuhiji maana siku moja Mwanasheria ananambia kwenda Makka ni kutembea nchi, kwenda kufanya hija na Mhe. Raza nitamchukua

na yeye. Kwa sababu unaposema ukweli siku zote unakuwa mtu mzuri kwa Mwenyezi Mungu tu, lakini kwa binadamu unakuwa mbaya, sijui kwa nini? Na kile kitu unachosema kina haki cha kuwasaidia wale wanyonge. Mimi nashangaa sana hebu nataka nitafute *definition* hii sijapata kwa Mwanasheria, sijapata kwa watu wa *laboratory*, sijapata kwa wanasayansi hiki kitu kinanipa tabu sana Mhe. Mwenyekiti, sijui mimi nimejaribu sana Mheshimiwa mimi sikusoma hapa, lakini siku moja nilijitangaza kuwa dokta watu wakakasirika, hapana, dokta ni mvumbuzi wa jambo si lazima u-*specialize*, ku-*specialize* ina *certificate* yake na ukiwa dokta mfumbuzi wa jambo ina *certificate* yake. Sasa mimi mfumbuzi wa mambo mimi siku-*specialize* bwana Mhe. Mwenyekiti hata kidogo, lakini ufumbuzi wangu utamshinda mtu mwenye PHD na ninamshinda kabisa na ningekuwa naye sambamba, lazima tuseme ukweli ulivyo.

Sasa Mheshimiwa kuna ujanja siku hizi wa Makampuni ufanye hivi, wanauziana makampuni, lakini wewe huoni jina linakuwa lile lile, lakini kampuni ishauzwa, sasa *in voice*, *in voice* inakuwa tofauti. Mheshimiwa angalia sana hii, Mrajis angalia hii tumeshapigwa changa la macho vibaya sana, mahoteli wanauziana makampuni kwa makampuni lakini ukiona jina lile lile utasema aa hakuna aa, na *management* utaikuta ile ile Mhe. Mwenyekiti, lakini twende kwenye makampuni utaambiwa kampuni hii *in voice* yake itumie, kwa *in voice* hii utakwenda kulipa katika *account* fulani.

Mhe. Mwenyekiti ni jambo ambalo linanisikitisha sana tumeshapoteza sisi mapato mengi sana Zanzibar, mimi naomba sana Mheshimiwa sheria sasa ifuate mkondo wake haraka sana wala tusiwaache watu kabisa. Kwa sababu ni kuokoa pato kumuokoa mnyonge wa Kizanzibari ili aweze kuondokana na umaskini kwa kuokoa hilo, najua hilo watu watanuna, potelea mbali na wanune lakini mimi ukweli nitausema, ni hatari nchi yetu hii inakufa umaskini watu wanatajirika watu wachache kwa michezo michezo tu hii, haiwezekani. Mheshimiwa naomba sana

Mungu anilinde na *inshaallah* Mungu atanilinda wala sitoogopa, ukweli nitausema lakini hii ndio hali halisi ilivyo.

Mheshimiwa mimi nakubaliana nayo na kama nilivyoeleza hivi, kampuni inaweza kwa azimio maalumu na kwa idhini ya maandishi ya Mrajis kubadilisha jina lake. Na nikisema naomba nipewe takwimu, naomba sana hiyo *serious* ya takwimu, kampuni ngapi zimefanya hivyo na kupelekewa Mrajis na Mrajis akakubali kuwa kampuni zibadilishwe jina moja hilo.

Pili, kwa hili niko *serious* kama Wizara itakuwa haina mafuta mimi niko tayari kutoa mafuta tukafanya uchunguzi katika mahoteli na wataona ukweli. Unajua Mhe. Mwenyekiti, jamani mimi siku zote nasema Waheshimiwa wenzangu Wawakilishi tumeapishwa kwa msahafu, na kila mtu aliyekuja hapa kaapa kwa mujibu wa dini yake na kajitia udhu kila mtu mwenyewe anajua jinsi alivyofanya. Mheshimiwa tukinyamaza kimya hatuyasemi haya mambo ambayo yanadhalilisha, msahafu utatuonea. Na ndio maana utakuta Waheshimiwa wengi tunaondoka hapa hatuna kitu kabisa, nyinyi mnafanya mchezo msahafu tulioapa chini ya ukumbi tukasema "*Wallahi laadhim*" halafu wewe unaona mambo hutaki kuyasema na unamwambia ee Mwenyezi Mungu ninakushirikisha, nitafanya kila unaloliona. Jamani tusifanye mchezo msahafu mbaya ule, mbaya wa kukuhukumu nimekusudia Mheshimiwa Mwenyekiti. Sio kama ni mbaya, mbaya wa kukuhukumu kwa sababu utakuhukumu wewe ule msahafu umefanya lipi na umekula kiapo na mambo umeyaona. Basi tuogope tusiwe Waheshimiwa wa kuvaa koti, na utekelezaji uwepo, sio mas-hara Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, hii hali ambayo ningesema inatudhalilisha kusema ukweli kuwaachia watu kila siku kukicha wanaonesha kuwa wamebadilisha jina kumbe hawajabadilisha jina, haiwezekani Mheshimiwa, naomba tuwe *serious*, na hii sheria tukiipitisha tuanze kazi mara moja Mheshimiwa ndio kazi ya msahafu unavyotaka.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda ukurasa huo wa 26 kifungu cha 18(3) "mabadiliko ya jina yaliyofanywa na kampuni chini ya kifungu hiki, hayataathiri haki yoyote au wajibu wowote wa kampuni au kuathiri taratibu zozote za kisheria za au dhidi ya kampuni na taratubu zozote za kisheria ambazo zinaendelezwa au kuanzishwa dhidi ya kampuni kwa jina lake la zamani zinaweza kuendelezwa au kuanzwa dhidi yake kwa jina lake jipya''

Mhe. Mwenyekiti, athari ipo hapa kwa sababu mtu anaweza akafanya mpango watu wawili tu wakaja wakaleta ubadilishaji wa jina wengine hawana habari na hiyo ni kweli, unajua kwenye kampuni mara nyingi wanatokea wajanja wanakuwa wawili hao ndio wanaojua mambo yote. Sasa hapa nataka nimwambie Mrajis asikubali sasa hivi, *people only two* wakienda katika ofisi yao wakasema aa sisi tunabadilisha, kwa hiyo barua yetu hii na nini, asikubali. Nimeshaona watu wengi imewaathiri hiyo, wanafanya hivyo kwa kuja tu pale na Mrajis masikini ya Mungu anakubali kwa sababu anaona kwa mujibu wa sheria imempa mamlaka hiyo, lakini kumbe kinyume chake kinakuwa kibaya.

Kwa hivyo, naomba sana hii sheria aiangalie vizuri Mheshimiwa, nakubaliana nayo sina tatizo, lakini awe makini sana kwa kuwa watu wachache tu wakija wasije na watu ambao wakasema tunabadilisha jina kumbe wengine hawana taarifa yoyote, na hatimaye wakaja wakakosa fursa ambazo wataweza kupata hisa zao. Wanaweza kuambiwa kwamba aah, kampuni mnayosema nyinyi iko wapi? Hii imeshapita zamani, sasa inakuwa wengine pale wameshapigwa bao hawana kitu walichopata na wameshafanya mambo mengi.

Nikiendelea katika ukurasa wa 29, kama mtu yeyote anauza au anaendesha biashara yoyote au taaluma yoyote chini ya jina la lakabu, hii lakabu *what is lakabu*, hebu naomba niambiwe Mhe. Waziri nisaidie labda *typewriter* au ndio jina la kisasa na hili

linatoka Arabian au linatoka wapi, naomba tafsiri yake hili neno lakabu ambayo ina neno hili la *limited*.

Kwa hivyo, Mheshimiwa naomba ufupisho wowote au kuiga neno hilo kwa kuwa na neno la mwisho mtu huyo isipokuwa kihalali kabla ameandikishwa kwa dhima yenye ukomo atakuwa amefanya makosa, lakini sioni hukumu yake inakuwaje Mheshimiwa, labda niendelee kuisoma, mtu ambaye si kampuni ya umma atakuwa amefanya kosa kama anauza bidhaa, taaluma na uendeshaji wa biashara yoyote chini ya jina ambalo linamjumuisha kama sehemu yake ya mwisho maneno ya kampuni ya umma yenye ukomo wa ufupisho wake wowote.

Mhe. Mwenyekiti, sijaona hukumu mimi hapa, anaambiwa amefanya makosa tu lakini anayefanya makosa nini hukumu yake, amefanya makosa kampuni itafutwa, amefanya makosa atatoa faini na atatiwa ndani, nini hukumu yake Mhe, Mwenyekiti? Naomba sana Mhe. Waziri aweze kunisaidia kwa sababu ni jambo kubwa sana. Siku hizi watu wanafanya mbinu, mtu anaweza akatangaza biashara jina la mtu mwengine mwenyewe hata ataposhtuka basi keshafilisiwa, atakuwa ameshapata faida yule aliyejitangazia.

Mhe. Mwenyekiti, naomba hili suala tuoneshwe, sheria hii ya kumtia mtu hatiani katika miaka hii mimi bado sijaona adhabu hii, na kama ipo ni adhabu gani ambayo inaweza ikamtia hatiani mtu. Naomba sana Mheshimiwa nisaidiwe, kwa sababu leo mimi sikuvaa miwani basi inawezekana Mhe. Waziri amekiweka kifungu hicho lakini kwa kuwa miwani nimeisahau nyumbani inawezekana ikawa sikukiona.

Nikiendekea Mhe. Mwenyekiti, wanavyosema wataalamu kuwa nikisema ukurasa wa 29 kifungu cha 21(1) inaeleza hiyo, wamesema wataalamu niwafafanulie Mhe. Mwenyekiti, sitaki nirejee hiki lakini wameniomba nikieleze kifungu hiki na kuna wengine labda wameingia sasa hivi hawakufahamu. Sasa

kifungu hicho na kifungu cha pili mtu ambaye si kampuni ya umma atakuwa amefanya kosa kama atauza bidhaa, taaluma na uendeshaji biashara yoyote chini ya jina ambalo linamjumuisha kama sehemu yake ya mwisho wa maneno kampuni ya umma yenye ukomo au ufupisho wake wowote. Hilo ni kosa unaambiwa lakini kosa lenyewe silioni uzito wake atafanya mtu wa biashara tu hizo.

Hapa leo nilimuuliza Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria swali la kuondolewa hukumu ya kifo tukaweka hukumu ya kufungwa maisha, nilikuwa nina sababu zangu kwa kichwa changu kinavyonieleza, tunaambiwa maraisi wengi wanashindwa kutia saini na ndio maana wenye kutia idhini ya kusema kifo hicho kihalalike ni maraisi, na wanachukua muda mwingi na yule mtu anakaa ndani muda mwingi, basi nikasema ile sentensi ibadilike itamke neno hilo. Sasa na hapa nasema Mheshimiwa nimeona kosa mtu katiwa hatiani lakini sioni hukumu yake, ningeomba sana nione hukumu ya huyu mtu kawekewa miaka mingapi, faini yake kiasi gani, mimi nitakuwa sina tatizo lakini kifungu hiki bado nina wasiwasi nacho hiki, naomba sana wataalamu wake kunitafsiria vizuri, sikipitishi kifungu hiki, mimi kama sijaona hukumu zake ziko wapi labda huko mbele nitakokwenda niweze kukuta suala hilo la hukumu.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 22 kinasema kwamba:

> “Bila ya kuathiri masharti ya sheria hii, katiba na kanuni, zikishasajiliwa, zitaifunga kampuni na wanachama wake kwa kiwango sawa kama kwamba zilitiwa saini na kila mwanachama na makubaliano yaliyomo ya kila mwanachama kuzingatia masharti yote ya katiba na ya kanuni”.

Mhe. Mwenyekiti naomba nisome tena kifungu hiki cha 22(1)

> “Bila ya kuathiri masharti ya sheria hii, katiba na kanuni, zikishasajiliwa, zitaifunga kampuni na

> wanachama wake kwa kiwango sawa kama kwamba zilitiwa saini na kila mwanachama na makubaliano yaliyomo ya kila mwanachama kuzingatia masharti yote ya katiba na ya kanuni".

Mhe. Mwenyekiti, akimalizia kifungu cha 22(2) kinasema kwamba

> "Fedha zozote zinazopaswa kulipwa na mwanachama yeyote wa kampuni kwa mujibu wa katiba au kanuni zitakuwa ni deni kutokana na yeye kwa kampuni hiyo".

Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki kidogo mimi sijakifahamu vizuri, nimuombe sana Mhe. Waziri sijui alikusudia kusema katika zile hisa zao ziwe sawa, au katika ule mchango wa fedha wanatakiwa zikishasainiwa katiba na kanuni asizidi mmoja akawa juu, hebu naomba nifahamishwe hili. Kwa sababu nina *experience* ya mambo mengi, mara nyingi kwenye makampuni watu hapa ndipo wanapofanya mchezo wa kudhulumiana. Mmoja anasema nimetoa nyingi, mwengine anasema hapana, madhali tumekubaliana hisa zetu ziwe sawa au mgao wetu, kwa hivyo tusitizame huko nyuma tunataka mgao uliokuwa sawa. Sasa ikiwa ndivyo kukubaliana huko sina tatizo na Mhe. Waziri itakuwa wametaka lile lengo la kumlinda yule mtu mnyonge aliyeingia katika kampuni ile na keshaoana kuna njia nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikwambie kweli sisi wengine tushaonewa sana kwenye makampuni. Mhe. Mwenyekiti, mimi nilijitia kwenye Kampuni ya *Sepideh,* kutokana na kutojua basi nimekwenda na maji. Kwa sababu kutojua sheria za kampuni kwa undani sijui haki yangu nitaipata wapi? Shilingi 66 milioni na zaidi sijui niende wapi nikadai. Sasa ndio maana mimi nikamshukuru sana Mhe. Waziri na Mrajis wake wametuletea hiki kitu cha kutufunua macho. Mheshimiwa sikondi tu, lakini ningekuwa nakonda kutokana na hilo jambo lililonikuta basi ningekonda, lakini Mwenyezi Mungu tu kanipa mbolea mwili

wangu *Alhamdullilah* mimi ndio niko hivi. Kutojua sheria basi nimedhulumiwa.

Sasa tahadhari hii isiwapate na wenzangu kudhulumiwa, niseme ukweli kwa nini nifiche? Leo nimezidiwa ujanja mtoto wa mjini nakubali hilo. Mimi Mheshimiwa hapa ndio nikaona kifungu hiki niking'ang'anie. Mhe. Mwenyekiti, kama kuna sheria naomba sana Mhe. Waziri na Mrajis waniokoe wanisaidie hii kampuni waibane nipate haki yangu *otherwise* nimekwenda na maji ndio sina uwezo tena wa kuzipata hizo. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Mwenyekiti, tuwe *serious* sana katika masuala kama haya ya kuwaelimisha wenzetu wadogo waliokuwa hawajui wasijiingize katika madimbwi, maana mimi niliona umasikini *bye bye* nilisema hata nisingegombea tena mara hii, lakini kumbe umerudi pale pale fyuu, fedha zimekwenda na maji hata pesa ya kampeni sina sasa hivi, maana yake zote wameshazichukua.

Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana, niwashukuru sana Mhe. Waziri na Katibu wake na Mrajis na Wakurugenzi wake wote na hiki ni kilio ambacho wananchi wa Jimbo la Kitope wanataka kuunda makampuni, lakini kumbe walikuwa hawajajua utaratibu ulivyo, na sasa hivi sheria kama inavyoletwa hapa kwa marekebisho, mimi niseme naunga mkono kwa asilimia thamanini ili sentensi nyengine nimalizie kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mheshimiwa nashukuru.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kupata fursa ya kuchangia mswada huu, Mswada wa Sheria ya Kampuni ya Mwaka 2012. Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nianze kwa kumshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kutuletea hii sheria hasa ukizingatia kwamba sheria hii ni ya zamani sana na inastahiki kutuletea hii sheria ili kuifuta baadhi ya vile vifungu na kufanya marekebisho mengine. Kwa sababu sheria ukiiangalia hasa ni sheria ya zamani sana, sheria yenyewe ni ya tangu mwaka 1948. Sasa mwaka huo mpaka leo mwaka 2013, ukiangalia hii sheria

ina zaidi ya miaka 60 mpaka 65 kwa hivyo ni kiasi kuletwa. Kwa kiasi fulani pamoja na kuwa wamechelewa lakini niwasifu sana kwa kuona kwamba kuna haja ya kutuletea hii sheria.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kumpongeza Mhe. Waziri kwa kutuletea hii sheria sasa naomba nimwambie Mhe. Waziri sheria kama hizi nzuri kabisa tumeshazipitisha nyingi. Hii sheria hasa ni nzuri, kwa sababu uzuri wake ime-*cover* kila kifungu kilichokuwa kina matatizo kimefutwa au kimewekwa upande kinawekwa kifungu ambacho ni kizuri.

Pia nisisahau kuwapongeza wenzetu wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala wamefanya kazi nzuri ya kurekebisha na kuweka sawa vifungu vya sheria ambavyo vilikuwa vina makosa na ambavyo vinataka kufanyiwa marekebisho wamefanya marekebisho. Kwa hivyo, wanastahiki hasa kupongezwa kwa sababu wamefanya kazi kubwa sana, ukiangalia katika marekebisho yao basi utaona wamefanya kazi kubwa na nzuri sana. Sasa Mhe. Waziri ninachomuomba mimi ni kwamba sisi hapa Zanzibar kila siku suala hili huwa nalisema, na leo nalisema tena, ni watu wazuri tu wa kutunga sheria, na sheria zetu tunazozitunga ingekuwa kuna nchi inachukua sheria zetu ikazifanyia kazi basi nchi hii ingekuwa ishasonga mbele na iko mbali sana kwa sababu tunatunga sheria nzuri, lakini tatizo kubwa ni utekelezaji wa sheria, tunatunga sheria lakini utekelezaji wake ni mgumu kabisa kwa sababu tunakuwa hatutekelezi zile sheria tukishazitunga.

Sasa namuomba Mhe. Waziri hii sheria tutaipitisha Wajumbe wote *Inshaallah*, na nawaomba kwa vile ni nzuri basi tuipitishe ili ilete faida kwa nchi yetu. Lakini namuomba sana Mhe. Waziri sheria hii tukishaipitisha basi aisimamie utekelezaji wake ili kuweza kutekeleza na kufanya kazi na kuleta faida katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, sheria hii imezungumza kuhusu masuala ya hisa, kama mtu yeyote yule hawezi kuongeza hisa ya mapato katika kampuni yake mpaka atakapopita kwa msajili na akaona kama kuna haja hiyo ya kuongeza hizo hisa za mapato ya nchi yetu. Kwa hivyo, hilo ni jambo zuri sana na nimpongeze Mhe. Waziri na namuomba lisimamiwe tuone kama hiyo faida inapatikana na serikali inapata mapato kutokana na hizi kampuni ambazo zitakuwa zinajisajili katika nchi yetu zinapewa usajili na zinafanya kazi kwa ajili ya kupata mapato.

Jambo jengine Mheshimiwa kuna vifungu ambavyo vimefutwa vile vya zamani vimewekwa vifungu ambavyo au sheria hii imerekebisha kuleta vifungu vipya. Hili ni suala zuri na Mhe. Waziri mimi sina budi nimpongeze, na nawaomba wenzangu kwa sababu hili suala linalofanywa hapa ni suala zuri basi tumpongeze na tuone kuwa ni mambo ambayo yanastahiki kufanywa.

Sheria hii pia Mhe. Mwenyekiti, zamani ilikuwa haitoi nafasi kwa mtu mmoja mmoja katika sheria iliyokuwepo ya zamani kuona kama mtu mmoja anaweza kuanzisha kampuni, ilikuwa kampuni ni yale makundi ya watu, lakini sasa sheria hii ya sasa inatoa nafasi hata kwa mtu mmoja kuanzisha Kampuni na akaweza kufanya kazi na akajulikana na sheria kama hii ni kampuni inafanya kazi.

Lakini kutokana na suala hili hili namuomba Mhe. Waziri labda anisaidie anipe ufafanuzi zaidi kwa sababu kidogo mimi nimepata utata, kwa hivyo aniweke wazi. Huyu mtu mmoja akiwa na kampuni yake itakuwa inaitwa ni kampuni ya mtu binafsi, lakini wakati huo huo kuna kampuni hizi zenye mikono ya serikali zinaitwa Kampuni za Umma, yaani ni kampuni lakini zilizokuwa zinatokana na mashirika ya umma. Sasa mimi namuomba Mhe. Waziri anisaidie kama mimi Subeit Khamis Faki mfano namchukua Mhe. Hassan Hamad Omar, Mhe. Ussi Jecha Simai, Mhe. Hamza Hassan Juma na zaidi Waheshimiwa

kama kumi lakini tunaanzisha kampuni yetu. Sasa je, itakuwa hii kampuni ni ya binafsi, ya umma au itakuwa na jina gani? Kwa sababu hii si ya mtu mmoja ni ya watu zaidi ya kumi itaitwa vipi kisheria? Ni ya umma, ya mtu binafsi au kampuni gani labda anisaidie hapo anipe ufafanuzi ili nipate uelewa zaidi, kwa sababu kidogo naona napata tabu sijajua mimi itakuwa ni kampuni ya aina gani kwa hiyo atusaidie Mhe. Waziri.

Suala jengine Mhe. Mwenyekiti, kuna sheria hii ya sasa inazungumza kama hizi kampuni zitakapokuwa zinatoa usajili sasa kuna kampuni hizi hazijalipa mapato, mfano ya serikali tuseme kwa Msajili wa hizi kampuni. Sheria inasema kama mtu huyu hatafuatiliwa lakini atasubiriwa mpaka pale atakapokuwa tayari anataka tena usajili wa mara ya pili sasa alipe mapato ya nyuma aliyokuwa akidaiwa madeni yake ndio sasa asajiliwe tena. Sasa utaratibu huu ni mzuri lakini mimi nilichokuwa namuomba Mhe. Waziri ni bora katika hizi kanuni zitakazotungwa za hii sheria basi ziwekwe sheria za kuwa huyu mtu asisubiriwe mpaka atakapokuja kusajili, kwa sababu ni sheria hii na kulipa ni sheria, basi kama ana madeni alipe asingojwe mpaka akakusanya madeni zaidi ya kumi tukajamlazimisha sasa kama alipe madeni yale yote ndio tumsajili pengine kampuni hii ikaja ikafilisika. Kwa sababu akilipa madeni ndio keshayakusanya mengi itakuwa kampuni haitafanya kazi, lakini iwepo sheria kwenye kanuni ya kumbana ili aendelee kulipa mapato yale ili ukija usajili basi asiwe na madeni makubwa aendelee na kampuni. Kwa sababu nia yetu ni kusajili kampuni nyingi ambazo zitakuwa zinaleta faida kwa wananchi na zinaleta mapato kwa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo nataka nilizungumze ni suala alilolizungumza Mhe. Makame Mshimba Mbarouk lakini na mimi nalitilia mkazo. Mhe. Mwenyekiti, elimu ni kitu muhimu sana, kwa hiyo naomba hii sheria yetu kwa vile ni nzuri sana Mhe. Waziri aandae programu nzuri kama ni kwa wafanyabiashara, taasisi, kwa watu binafsi, lakini watu wapewe

elimu kutokana na hii sheria ili hizi kampuni zisione uzito na zijue kama sasa hivi kuna sheria ambayo inazungumza kitu fulani. Kwa sababu watu wakipata elimu basi itakuwa ni vizuri zaidi kuliko hivi ilivyo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri alione kama hili suala la kutoa elimu ni suala zuri na alipe umuhimu wake ili sheria hii itakapokuwa tayari sasa basi watu waone kuwa hii sheria yetu ni nzuri na waje kwa haraka na waweze kufanya kazi na kuleta mafanikio zaidi kwa ajili ya sheria yetu na kwa ajili ya kupata mapato ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, sheria ni nzuri na kwa sababu ni nzuri sioni kama kuna mambo ya *query* nyingi ambazo zitazungumzwa, kwa sababu sheria ni nzuri. Sheria imeandikwa kitaalamu na imejengeka, imeandikika na imesomwa na imesomeka. Kwa hivyo, Mheshimiwa mimi nilikuwa na hayo machache ya kuchangia na naunga mkono hoja hii na nawaomba wenzangu tuiunge mkono kwa sababu ni sheria nzuri. Ahsante.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwanza nataka nikushukuru kunipa nafasi hii nikazungumzia kijumla jumla mswada huu ambao unasomeka kwamba ni Mswada wa Sheria ya Kampuni ya Mwaka 2012.

Mhe. Mwenyekiti, kama Waziri alivyosema kwamba sheria hii sio mpya, hii sheria ilikuwepo tangu wakati wa utawala wa Uingereza au tumeirithi kutoka kwa Waingereza na ikafanyiwa tena marekebisho na hivi sasa tunaiboresha zaidi ili iweze kwenda na wakati. Hii imetokana na aidha pengine michango mbali mbali inayotolewa na Waheshimiwa hapa Barazani au pengine malalamiko ya baadhi ya wafanyabiashara wenye makampuni pengine wanapata tabu katika shughuli zao mbali mbali katika utekelezaji wa majukumu yao.

Kwa hiyo, kutokana na usikivu wa Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wa wizara wameamua kwa makusudi kutuletea Mswada huu wa Sheria ili kuweza kurekebisha ule ugumu

ambao unaosababisha matatizo katika uwekezaji kwa upande wa Zanzibar, hasa kwa makampuni na kuweza kutengeneza sheria itakayoweza kurahisisha.

Mimi kwanza nataka nipongeze hasa kwa lile eneo ambalo ninalozungumzia kuhusu suala la masharti ya uanzishwaji wa kampuni kwamba si lazima ianzie kama ilivyokuwa inasema ile sheria ya mwanzo kwamba ianzie na watu wawili. Kwa sababu kama tunavyofahamu kwamba kampuni ni taasisi na kampuni ni taasisi yenye malengo maalumu. Sasa kama kuna mtu ambaye atakuwa na uwezo au mtaji wa kuweza kuanzisha kampuni na kuweza kutimiza yale malengo kwa mujibu wa sheria iliyokuwepo mimi nadhani hicho kikwazo kitakuwa kimeondoka. Kama tunavyofahamu kwamba nchi yetu hii Zanzibar ni nchi ya visiwa, na hatuna ardhi kubwa sana ya kilimo. Kwa hivyo, rasilimali yetu kubwa ambayo tunaitegemea zaidi ni wafanyabiashara ikiwemo Sekta ya Utalii. Hayo ndio mategemeo yetu makubwa.

Kwa hivyo, kurekebisha sheria hii ya Uanzishwaji wa Makampuni basi nadhani itaweza kusaidia kuongeza wigo wa watu kuendelea kujitokeza kuanzisha makampuni ili kuweza kutoa ajira kwa wananchi wetu.

Sasa mimi nilikuwa nataka nimuombe sana Mhe. Waziri kwa kushirikiana na Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko. Kitu ninachotaka kuwashauri ni kwamba Zanzibar nchi yetu ni ndogo sana, kwa bahati nzuri sisi tunazaa sana, nchi ni ndogo lakini tunazaa sana. Kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti, inapokuwa nchi yetu ndogo na tunazaa sana na vyuo sasa hivi tumejenga Vyuo Vikuu, hapa tuna wataalamu au wasomi wengi wanategemea kuja kuingia katika soko la kutafuta ajira. Ukiangalia serikali yetu tunamshukuru Rais wetu kafanya jitihada kwamba serikali yetu ni pana sana, lakini hii serikali haiwezi ikawa kila siku inanyumburuka, lazima kuwe na *limitation* yake. Sasa baada ya hizi wizara tulizokuwanazo

sitegemei kwa kuwa wananchi watakuwa wanadai ajira huko mitaani, serikali ianzishe wizara nyengine ili tuweze kuwa na hizo ajira. Lakini cha kufanya ni kujaribu kutoa semina hasa kwa wanafunzi wetu wa Vyuo Vikuu, kutoa semina kwa wanafunzi hao kujiandaa kuanzisha makampuni mara tu baada ya kumaliza vyuo.

Kwa sababu kuanzisha kampuni kunaweza kuwa huna hata shilingi, lakini unaweza ukawa na maarifa ya kufungua kampuni na yale maarifa yako yakakuwezesha kupata fedha katika taasisi za fedha ili sasa kuandaa hiyo timu ya *management* ikaweza kuendesha hiyo shughuli yao. Sasa fursa hii kwa vijana wetu wasomi hii ni fursa pekee kabisa, kwa sababu kama nilivyosema kwa kutegemea kwamba kila ambao wanaotoka vyuoni na mbali wale wanaomaliza pengine *Form II* wote wale wanakuja kutafuta ajira. Ukiangalia serikali wizara zetu zote zimejaa lakini vile vile hatuna makampuni ya kutosha. Kwa hivyo, fursa ya ajira iliyokuwepo ni vijana wetu walioko katika vyuo ambao wakipata semina nzuri, *course* nzuri ya masuala ya *management*, mimi nadhani itakuwa ni wepesi kuja kuanzisha hizo kampuni.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia Zanzibar hayo makampuni yaliyokuwepo kwa kweli ndio watu katika ile kuhangaika hangaika wanakuwa hawajui nini cha kufanya, kama ukiangalia kwamba kuanzisha kampuni angalau yule mwenye kampuni awe na taaluma ya biashara. Kwa hivyo, kuna wengine wanaanzisha makampuni lakini hata hiyo elimu ya biashara wanakuwa hawana, matokeo yake hata uendeshaji wa kampuni zenyewe zinakuwa zinakwenda kienyeji enyeji. Lakini kama nilivyoshauri kama tutawaandaa vijana wetu hawa wa vyuo wakaweza kupata mafunzo mapema ule mwaka wa mwisho wanatarajia kumaliza masomo yao wanafundishwa namna ya kuunganisha nguvu zao, kuandika miradi na kuweza kuanzisha kampuni. Sasa kwa kuwa wao ni wasomi wataangalia zile fursa vile vile zilizokuwemo katika visiwa vyetu hivi vya Unguja na Pemba ili kujua kwamba tukianzisha kampuni hii basi na kazi za kufanya zitaweza

kupatikana. Hiyo mimi nadhani katika muelekeo wetu wa baadae huko ndio kutiliwe mkazo mkubwa sana.

Lakini chengine Mhe. Mwenyekiti kuanzisha haya Makampuni vile vile kuwa na taratibu zake na kwa kuwa hapa tunarekebisha sheria ya kuanzisha haya makampuni naomba basi mpaka na yale masharti mengine kwa kweli yaweze kutiliwa mkazo. Na masharti mengine yepi, unajua sasa Mhe. Mwenyekiti uendeshaji wa makampuni wa sasa hivi tafauti na miaka iliyopita ya zamani. Sasa hivi unaanzisha kampuni, na kampuni inakuwa ni ya kwako au ni yenu nyinyi ambao mliojikusanya. Lakini wale wafanyakazi ambao mliowaajiri na wao wale wana haki zao za kimsingi katika kampuni. Kwa sababu bila ya wafanyakazi hiyo kampuni yako isingeweza kufanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, na wanaofanikisha malengo ya kampuni hiyo ni wale wafanyakazi ambao wanafanya kazi. Sasa kunakuwa na malalamiko yanakuwa yanajitokeza hapa na pale, na kuna mambo mengine Waheshimiwa mbali mbali wamekuwa wakiyazungumza hapa kwamba baadhi ya makampuni kutowatendea haki wafanyakazi wao. Sasa hili mimi nadhani katika sheria hii naamini kutakuwa na vifungu, lakini kama alivyosema Mhe. Subeit Khamis Faki kwamba hizi sheria tunazozitunga sasa basi hebu tujaribuni zaidi kuzisimamia ili watekeleze yale masharti yaliyomo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano sasa hivi kuna Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii yanatakiwa makampuni yote mpaka ya serikali kuwafungulia hisa katika Mfuko wa Hifadhi wa Jamii, lakini bado kuna baadhi ya malalamiko kwamba kuna baadhi ya makampuni wale wafanyakazi wao pengine kampuni ile inafika kufungwa basi wanapokwenda katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wanaambiwa kuwa michango yao haikupelekwa. Sasa hichi ni kitu ambacho kinachotakiwa lazima kwa yeyote anayeanzisha makampuni basi moja katika sharti hili na wao waweze kuwekewa. Kwa sababu

huu Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ndio utakaokuja kumfaa pale ambapo atakuwa tena hana nguvu za kufanya kazi, lakini chengine kuwe na masharti ya kulazimisha kwamba katika kila kampuni wale wafanyakazi basi kuwa aidha na tawi lao au kuwa na Jumuiya yao ya wafanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, hili kwa nini nalizungumza? Hili najaribu kulizungumza Mhe. Mwenyekiti kwamba kutokana na uhaba ya ajira au uchache wa ajira uliokuwepo kwenye visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Matokezeo yake wananchi wetu wanaposikia kuna sehemu kuna kampuni imefunguliwa wanataka wafanyakazi, basi vijana wetu wale hawaulizi unajua mtu kwenye njaa haulizi anasubiri mpaka yameshamkuta tena kama rafiki yangu hapa Mhe. Makame Mshimba Mbarouk tena ndio analalamika.

Sasa kitu ambacho kinachofanyika ni nini? Watu wale wanakwenda kampuni ile imekuwa *registered* katika serikali ni kampuni halali kabisa, lakini tatizo linaanza katika utaratibu wa uajiri. Sasa humu katika hii sheria katika uanzishwaji wa hii kampuni. Mimi nadhani yangeliwekewa vile vile na masharti ya uajiri. Leo wafanyakazi wetu katika makampuni yetu haya ya kawaida hawana mikataba ya kazi, lakini sasa kama katika sheria hii tumeweka kipengele cha kwamba kampuni yoyote itakayoundwa basi lazima kuwe na kipengele cha mkataba wa kazi na muwekezaji yeyote au kampuni yoyote itakayoshindwa kuwajazisha watu mkataba basi kampuni hiyo itakuwa imevunja sheria, na kuna kifungu cha adhabu kiweko kabisa kwa ile kampuni yoyote itayowaajiri wafanyakazi bila ya kuwa na mkataba.

Mhe. Mwenyekiti, vyenginevyo tutakuwa tunatunga sheria lakini hatukuwalinda watu wetu na sheria yoyote Mhe. Mwenyekiti, inavyotakiwa katika nchi alizungumza Dr Makame Mshimba Mbarouk ingawa hamtaki kumuita Dr. lakini mimi namwita Dr Makame Mshimba Mbarouk. Alizungumza kwamba sisi

tulipokuja hapa Barazani kabla ya kupewa ile sheria ya kinga na masharti basi tukalishwa kiapo pale tukaukamata msahafu. Sisi tumeukamata msahafu kwa kutetea maslahi ya wananchi wa Zanzibar. Na Katiba nyengine ya Jamhuri ya Muungano tumeapa kuyalinda maslahi ya wananchi wengine wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa tukishindwa kuwalinda katika maslahi yao katika ajira msahafu utatuchapa.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk alizungumza msahafu mbaya sana. Mimi nasema msahafu mzuri sana, yeye alizungumza ile lugha ya mitaani, lakini mitaani mtu anakutukana lakini ndio anakusifu na wewe mwenyewe unaridhika, sitaki kurejea kwa sababu tunajua tunavyosifiana huko mitaani.

Sasa yeye alizungumza msahafu mbaya sana kwa sababu mbaya vipi kwamba ule ukiutendea kinyume basi adhabu zake zitakushukia. Sasa sisi kwa kuwa tumekula kiapo hapo cha kuwatetea wananchi basi mimi nadhani kama kifungu hiki hakimo basi Mhe. Waziri tutafute eneo la kuweka masharti ya kwamba haya makampuni yoyote ambayo yatakayopata usajili katika yale masharti ya kuweka usajili wa makampuni basi lazima kuwe na kifungu kinachosema kutoa mikataba ya kazi. Kwa sababu ule mkataba wa kazi ndio unaoeleza haki zake zote; kuingia kazini, kutoka, maslahi yake anapostaafu, haki zake atazipata vipi. Kwa hivyo, hayo ni mambo ambayo ni muhimu sana.

Lakini kama nilivyosema kuwe na masharti ya vyama vya wafanyakazi. Kama nilivyosema hapo mwanzo wananchi wetu wengi wanapokwenda kuajiriwa katika makampuni kwa kuwa mtu hana kitu, kwa hiyo wala haulizi yale masharti yaliyopo, lakini kwa kuwa kutakuwa na Chama cha Wafanyakazi ina maana pale kutakuwa na uongozi wa kampuni, kuna uongozi wa wale wafanyakazi, lakini vile vile kutakuwa na mkono wa serikali kupitia Kamisheni ya Kazi ili sasa linapotokezea jambo lolote isiwe mwenye kampuni kuwafukuza ovyo wafanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi jambo lililojitokeza kwamba mtu anapokuwa anadai haki zake tena kwa kufuata taratibu basi unaweza ukakuta Meneja au uongozi wa ile kampuni wanamfukuza mfanyakazi Yule, na wakimfukuza mfanyakazi yule ina maana wale wafanyakazi wengine waliobakia hawatothubutu tena kunyanyua mdomo kudai haki zao. Kwa hivyo, hili kwa kweli linakuwa ni tatizo na ndio maana Mhe. Mwenyekiti, wafanyakazi wengi hasa katika Sekta ya Utalii katika mahoteli wengi huwa wanatupigia simu wanatufuata ili kutupa malalamiko yao kwa ule unyanyasaji wakati mwengine unavyofanyika katika sehemu zao.

Sasa hii inatokana na nini? Inawezekana aidha kuna Chama cha Wafanyakazi kilichokuwepo pale hakina nguvu, na pengine hakina nguvu kwa sababu wanajua kwamba wale wenye kampuni nguvu yao ni kubwa. Wale wanapodai maslahi yao wanaweza kuwafukuza. Kwa hivyo, ina maana hata yule Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyakazi katika kampuni ile na yeye anakuwa ni sehemu ya ile kampuni. Kwa hivyo, matokezeo yake yule Mwenyekiti wa Jumuiya ya wafanyakazi au Chama cha Wafanyakazi katika kampuni fulani anashindwa sasa kutetea maslahi ya wafanyakazi.

Sasa mimi nadhani mambo kama haya ukiyaweka katika sheria, kwa sababu tusihamasishe tu kurekebisha hizi sheria, lakini vile vile na kuweka mazingira ya kuwalinda wafanyakazi katika kampuni ile.

Chengine Mhe. Mwenyekiti, tusitetee tu wafanyakazi lakini tujaribu kuzungumza na wajibu wa serikali katika kuyalinda na kuyahifadhi na kuyahamasisha makampuni kuja kujisajili Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, utakuta kwamba serikali sisi Wawakilishi ndio tulioipitishia bajeti hapa kila mwaka ili kwenda kuwatumikia wananchi wetu, aidha katika kutoa huduma

za afya, pengine huduma za maji na nyengine mbalimbali pamoja na za maendeleo.

Sasa wakati mwengine kuna makampuni yanaanzishwa yanakufa kwa sababu mtu yeyote anapoanzisha kitu hasa kampuni anakuwa tayari ameshaangalia mtazamo wa mbele kwamba mimi nikianzisha kampuni hii kuna fursa moja, mbili, tatu nitaweza kuzipata kutoka serikalini. Kwa sababu ninapoanzisha kampuni mimi nitalipa usajili na kila kitu, lakini vile vile nitaajiri wafanyakazi nitawalipa vile vile. Sasa leo inapotokezea kazi ikiwa serikali haikuangalia kuwapa *priority* yale makampuni ya ndani.

Kwa hiyo, ina maana hii ni sawa sawa kusema yale makampuni tumeyaanzisha Jangwani. Kwa sababu kuyatilia mbolea serikali ndio yenye uwezo wa kuyatilia mbolea. Miradi yote inayofanyika Zanzibar lazima bajeti yake ipite ndani ya Baraza la Wawakilishi, na sisi mishihara yetu pamoja na wananchi wetu wa Zanzibar inatokana na kodi. Miongoni mwa kodi ni hizo kodi ambazo za hawa wanaoanzisha makampuni.

Kwa hiyo, ni busara sana kuweza kuangalia zaidi makampuni yaliyokuwa *registered* Zanzibar ili sasa kuweza kuwapa kazi ili hao vijana wetu waendelee kufanya kazi. Lakini na makampuni yapate faida ili yaweze kutanuka kuweza kuongeza ajira katika nchi yetu. Vyenginevyo Mhe. Mwenyekiti tutakuwa tunaimarisha makampuni ya nje, akishamaliza kazi zake ameondoka na yale makampuni yetu ya ndani yakishafungwa yote hawa vijana wetu sijui atakuja kuwaajiri nani?

Sasa nilikuwa naomba sana serikali yetu ijaribu sana kuyalinda haya makampuni yetu ya ndani, lakini vile vile kuwapa fursa za kuweza kupata miradi mbali mbali ya kuweza kufanya kazi ndani ya serikali ili makampuni yale kuweza kuhuika.
Mhe Mwenyekiti, vile vile ni wajibu wa serikali yetu mpaka sasa hivi Zanzibar hatuna Benki ya Uwekezaji. Hili ingawa kidogo

itakuwa liko nje ya hii sheria, lakini leo tunapohamasisha au tunarekebisha sheria ya uwekezaji. Lakini vile vile tutengeneze mazingira ya kuongeza hayo makampuni ambayo yatakayokuja kuwekeza Zanzibar.

Kwa hiyo, ni busara ili haya makampuni yetu yawe mengi na *active* basi ni vizuri serikali yetu ikaangalia uwezekano wa kuanzisha Benki ya Uwekezaji ambayo wenzetu kwa upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tayari wanayo inaitwa *Tanzania Investment Bank* ambayo hawa wenye makampuni wanapata nafasi ya kuweza kuimarishaa mitaji yao.

Sasa na sisi Zanzibar ni vizuri taasisi kama hizi tukawa tunazo ili kuweza kuwahamasisha hawa wananchi wa kawaida au makampuni ili kuanzisha hizo kampuni. Kwa sababu mfano kama ule nilioutoa mwanzo Mhe. Mwenyekiti, leo ukiwatoa wanafunzi *fresh* kutoka vyuo tayari umeshawapa taaluma ya kuweza kuanzisha kampuni zao elimu wanazo wanaweza wakajikusanya katika watu tafauti. Lakini je, *capital* wataipata wapi?

Tukiwa na benki ambayo itakuwa *Zanzibar Investment Bank* hiyo itakuwa ndio njia ya kuwapeleka wao kuweza kumudu kuanzisha hizo kampuni. Kwa hivyo, ndio maana nikasema hivyo, pamoja kwamba tunarekebisha sheria hii lakini vile vile tutengeneze mazingira ya kuweza kutoa nafasi nzuri kwa makampuni kuweza kuwekeza kwa hapa Zanzibar.

Jengine wakati mwengine wananchi wetu wanaanzisha kampuni. Lakini kampuni hizi pengine kutokana na kuwa na maarifa madogo ya kuweza kuimarisha zile kampuni zao. Matokeo yake utakuta kuna kazi zinachukuliwa na kampuni za kigeni ambao wao vijana wetu au wananchi wetu wa Zanzibar wanakuwa wana uwezo wa kuanzisha na kuboresha kampuni zile ili kuweza kuendana na soko lililokuwepo. Kwa mfano Mhe. Mwenyekiti, wako wenzetu wengine askari wastaafu, wengine watu tu wa

kawaida kutokana na haja ya soko yaani kutokana na hasa vitendo vinavyofanyika vya uhalifu na mambo mengine wameamua kwa makusudi kuanzisha makampuni ya ulinzi.

Kwa hivyo, wanaanzisha makampuni yale ya ulinzi wanawachukua wale askari wastaafu wanawaajiri, wengine wanawaajiri vijana *fresh* wengine wakishatoka JKU au JKT hawajapata ajira wanawaajiri, lakini unaweza ukakuta soko kubwa katika eneo hili la ulinzi basi unaweza ukakuta linachukuliwa na kampuni ambayo siyo ya hapa nchini, unaweza ukaikuta kampuni pengine kutoka Kenya wao wamechukua nafasi mfano katika *security.* Sasa utakuta mambo kama haya Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli yanapunguza ari ya wale watu wetu kuweza kutanua zile shughuli zao, na utakuta wakati mwengine wanashindwa pengine mtaji tu pengine wa kutafuta sare, viatu lakini pamoja na suala la usafiri, lakini kwa sheria hii nadhani itaweza kusaidia hayo mengine yataweza kujirekebisha kwa sasa hivi na hii sheria basi hata wale wenzetu wenye taasisi za kifedha basi kwa kuangalia kama wawekezaji ambao wameanzisha hizi kampuni hasa hawa wazalendo kama wamekuwa na uwezo wa kuanzisha hizo kampuni basi vile vile kuwapa wepesi kwa kutumia sheria hii na wametimiza yale masharti waweze kupatiwa mikopo kwa ajili ya huduma zao.

Maana yake kwa mfano kuna makampuni ya ulinzi haya. Kampuni ya ulinzi inatakiwa iwe na gari, pikipiki, lakini vile vile wawe na *Radio call*. Wawe na uwezo wa kuweka minara yao ambayo wataweza kufanya mawasiliano, lakini sasa kampuni zetu za kizalendo hasa hapa Zanzibar bado utakuta uwezo huu na maarifa haya wanakuwa hawana. Kwa hiyo, matokeo yake zile kazi zinachukuliwa na kampuni nyengine za nje.

La mwisho Mhe. Mwenyekiti, ili na wenzangu niwape nafasi waweze kuchangia nataka nizungumzie suala la Kampuni ya Zantel.

Mhe. Mwenyekiti, kampuni hii hichi kipindi cha kati imekuwa ikipata misukosuko mingi sana na ilifika pahala hata zile kodi kwa sababu hii kampuni imesajiliwa Zanzibar na kuna hisa za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar vile vile, lakini walifika pahala wakatikiswatikiswa ili kodi zao wasilipie hapa Zanzibar.
Sasa hivi sheria kama ninavyosema pamoja na kwamba tunazitunga pamoja ili kuweza kuyavutia makampuni kuweza kuja kuwekeza Zanzibar. Kwa hivyo, na nguvu kama hizi kampuni yenyewe kama kampuni kwa kweli uwezo wa kupambana unakuwa ni mdogo. Kwa hivyo, hapa eneo kama hili serikali lazima iingize mkono wake. Vyenginevyo mfano leo Kampuni ya Zantel ikishindwa kuhimili vishindo vya *TRA* wakaweza ku- *surrender* kodi yao wasilipe Zanzibar tusitegemee kama kuna kampuni nyengine yoyote ya simu kubwa kama itakuwa na uwezo au watakuja kuwekeza Zanzibar.

Kwa hivyo, ndio maana nikasema ni vizuri serikali yetu tukatengeneza mazingira ya kuyalinda yale makampuni ambayo tayari tunayo, wanapopata misukosuko hasa yale ambayo kuna nguvu kubwa za serikali basi serikali yenyewe inatakiwa iingilie ule usajili wao wa kampuni kwa hapa Zanzibar waone kwamba unathaminiwa, lakini vile vile na wao wanapopata matatizo kuweza serikali kuwatetea.

Sasa mimi kama nilivyosema hapa mwanzo kimsingi nilikuwa sina mambo makubwa, kwa sababu najua Kamati wamepitia kuna marekebisho mengi kwenye tafsiri tumejaribu kuangalia wamejitahidi wamefanya marekebisho mengi sana.

Lakini vile vile ningeliwaomba na Wajumbe wa hizi Kamati na hili nalizungumza nikiwa ndio Mwenyekiti wa Wenyeviti wote wa Baraza la Wawakilishi wa Kamati. Nawaomba sana Wajumbe wa Kamati hii miswada sisi tunapitisha sheria, na sheria hizi zinakwenda kuwatawala wananchi wetu. Wananchi wetu wengi sana au wengi wao hawapati nafasi ya kuisoma hii miswada. Kwa hiyo, wale Wajumbe wa ile Kamati ambao

wanashiriki kuanzia mwanzo toka mswada unakwenda kwenye Kamati kabla haujaja Barazani.

Mswada unapokwenda kwenye Kamati wanapata maelezo ya Waziri, wanapata maelezo ya wataalamu, wanawaita wadau, wadau wale wanachangia mawazo yao. Sasa yale waliyoyapata waje watusaidie na sisi hapa Barazani, lakini leo ikiwa Mwenyekiti akishasoma wale Wajumbe wa Kamati wanaingia mitini, mimi nafikiri hatutendeani haki.

Kwa sababu huu mswada sio kupitisha tu vifungu lakini unapochangia na ukakosea vifungu ukarekebisha kifungu hata wale wadau mliowaalika yale mawazo yao waliyoyatoa unaweza ukanukuu kwamba wazo hili tulipata kwa wadau wenyewe, na wao wanafarijika kwamba yale mawazo tuliyoyapeleka kwenye kamati, kamati imeyathamini na yamechangiwa na pengine yameingia katika sheria.

Sasa mimi nilikuwa naomba sana wenye Kamati sheria yoyote kama na sisi tunavyowalazimisha Mawaziri siku ya mswada wake awepo mwenyewe basi tunawataja, na Wajumbe wote wa kamati siku ambayo mswada wao wa wizara yao unawasilishwa wawepo wote kuanzia mwanzo mpaka mwisho. Kwa sababu kuna baadhi ya mambo mengine sisi ambao hatukushiriki katika Kamati tunaweza tukahoji, lakini kwa kuwa wale Wajumbe wenzetu wa kamati walikuwemo wataweza kutusaidia kutoa ufafanuzi, lakini vile vile kumpunguzia kazi Mhe. Waziri ya kuja kujibu yale masuala yetu.

Sasa mimi nadhani hili natoa wito tu kwa Wajumbe wenzangu wa Kamati basi tusaidiane tu, na hii tunaposema kwa sababu mswada huu ukishakuja hapa Mswada wa Serikali. Lakini huu unakuwa tena si Mswada wa Serikali huu mswada unakuwa ni mswada wa Baraza la Wawakilishi, na ndio maana hii sheria inapotungwa unaambiwa imetungwa na Baraza la Wawakilishi. Waziri akishauleta tu Barazani inakuwa si mali yake inakuwa

mali yetu, sasa sisi tumsaidie kuuchangia ili tumpelekee Mhe. Rais aende akautie saini mswada ambao umeshaboreka.

Sasa baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura tunauunga mkono mswada huu, na wameniomba tu jioni Mhe. Mwenyekiti uturuhusu ili tukaungane na wananchi wetu kwa maandalizi ya sikukuu ya Eid Elhaj. Kwa sababu leo Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema ukiwa kama Mwenyekiti wa Wenyeviti unabebeshwa mambo mengi.

Sasa hili lilikuwa ni ombi pamoja kwamba ni ombi la wananchi wa jimbo la Kwamtipura, lakini naamini na Waheshimiwa wengine wana majimbo vile vile walikuwa wanahisi wanawahitaji Waheshimiwa wao jioni ya leo ili wakakae nao pamoja kwa maandalizi ya sikukuu kubwa ya Eid Elhaj.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naamini na hayo mapendekezo yangu utayazingatia nakushukuru sana, naunga mkono kwa asilimia mia moja. (*Makofi*).

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuchangia hoja ilioko mbele yetu nimalizie pale alipomalizia Mwenyekiti wangu Mhe. Hamza Hassan Juma si wapiga kura wake yeye tu, lakini vile vile wapiga kura wa Wawi kesho wanatamani wale sikukuu na Mwakilishi wao hasa ukiangalia kwamba ndege za kuelekea Pemba zinamalizikia saa 10:00 pale, kuita Baraza saa 11:00 ni kuwanyima haki yao ya msingi wapiga kura wa jimbo la Wawi kula sikukuu na Mwakilishi wao.

Kwa hivyo, kwa heshima kubwa na unyenyekevu wa hali ya juu Mhe. Mwenyekiti wapiga kura wa Wawi wanakuomba mara tu tukimaliza asubuhi umtake Mwanasheria Mkuu wa Serikali aweze kuakhirisha kikao ili tusishiriki katika Baraza leo jioni ili

tuweze kusafiri kwenda Pemba wengine kwenda kula sikukuu na wapiga kura wetu wa Micheweni, Kojani,Wawi na kadhalika Mhe. Mwenyekiti. Baada ya maelezo hayo naomba sasa niende katika hoja ilioko mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru na mimi kwa kunipatia nafasi ya kueleza machache sana juu ya hoja hii ilioko mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze serikali kwa kuweza kuleta mswada huu. Mswada huu mimi naona umechelewa sana kuletwa mbele yetu kwa sababu sheria iliyokuwa inashughulikia mambo haya ni kongwe sana. Hii ni tangu mwaka 1948 ndio ilikuwa ikushughulikia mambo ya uanzishwaji wa Kampuni ni kongwe mno. Kwa hivyo, mimi naona serikali imechelewa kuleta mswada huu, lakini kwa sababu umeletwa lazima niipongeze serikali.

Mhe. Mwenyekiti kabla sheria hii kuletwa kwa kweli katika nchi hii kulikuwa na mambo ya ajabu sana. Kulikuwa na watu wana uwezo wa kufanya biashara kama wao, wana uwezo wa kufanya biashara kama makampuni, lakini kwa kweli ilikuwa wakipata madhila makubwa kwa serikali. Sasa nadhani kuletwa kwa sheria hii inaweza kuwa mkombozi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi katika miaka ya 70 mwishoni hapa nilikuwa na uwezo wa kufanya biashara sana hapa katika nchi hii, na nilikuwa na uwezo wa kusafiri baina ya Unguja na Pemba baina ya Unguja na Dar es Salaam baina ya Unguja na Mombasa pale kwa ajili ya kufanya biashara kwa ajili ya maslahi yangu ya nchi yangu na ya wananchi kwa ujumla. Lakini kwa sababu hakukuwa na sheria makini inayosimamia masuala ya biashara Mhe. Mwenyekiti wengi wetu sisi tulikamatwa kama wahujumu wa uchumi. Mimi nadhani sheria ikaweka mazingira mazuri ya sisi wafanyabiashara kuweza kufanya biashara zetu vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, bila shaka sheria hii kwa upande mwengine itakuwa ni mkombozi, kwa sababu sheria inayopitwa na muda wake ilikuwa haitoi viwango vya biashara aidha zinazoingia au kutoka katika nchi yetu, lakini kwa sababu tayari mswada naamini kwamba viwango vya kuingiza biashara na kutoa biashara katika nchi vikawekwa katika umakini wa hali ya juu, jambo ambalo sio tu kama litainua uchumi wa nchi hii, lakini vile vile litaweka hadhi za bidhaa za nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kutokuwepo kwa sheria hii katika kipindi kirefu kwa kweli kumerudisha nyuma sana uchumi wa nchi yetu na wafanyabishara wa nchi yetu kwa sababu kulikuwa hakuna chombo kilichokuwa kina ubora. Sisi tulikuwa tunasafirisha embe mwarugo hizi zinahitajika sana katika nchi hizi za falme za kiarabu Mhe. Mwenyekiti. Sisi tulikuwa tunasafirisha mapapai kutoka maeneo ya maweni kule kwao Mhe. Hija Hasssan Hija, tukisafirisha mapapai kutoka maeneo ya Matemwe kupeleka katika nchi za falme za kiarabu kwa bei nzuri sana, na walikuwa wakiyapenda sana mapapai ya Zanzibar.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, la kusikitisha sasa zile embe mwarugo zilikuwa zikitafutwa tu huko Dar es Saalam watu wanajipanga jipanga humo wanaziita mwarugo huku zina mafunza. Matokeo yake embe zile sasa hivi hatusafirishi tena hazitakiwi tena na zimepoteza sifa yake sio zile embe tu, lakini zimepoteza sifa za embe za mwarugo kutoka Zanzibar.

Kwa hivyo, sheria hii naamini kuwepo kwake Mhe. Mwenyekiti, bidhaa zetu zile zinazosafirishwa zitaweza kuwa na viwango vyake. Maana yake mwarugo inayozalishwa Muyuni, inazalishwa Chonga pale Chanja Mjawiri nakuhakikishia Mhe. Mwenyekiti, katika ulimwengu mzima hakuna. Bara wenzetu wamezitohoa tohoa huko, sasa sisi hatuuzi na wao hawauzi. Kwa hivyo, naamini sheria hii itazidhibiti bidhaa zetu hizi.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo jengine lililokuwepo kabla ya sheria hii ni kwamba wafanyabiashara walikuwa wanaingiza bidhaa zilizokuwa sio tu kwamba hazina viwango lakini hata baadhi ya biashara za hatari wakati mwengine. Sasa nilikuwa nataka Mhe. Waziri atakaposimama hapo anifafanulie kuna wafanyabiashara katika wananchi kadhaa sijui hapa kwetu Zanzibar. Lakini waliingiza maziwa kama miaka miwili iliyopita nyuma maziwa ya unga yale kutoka China ambayo yana *Cyanide*. Sasa bidhaa kama zile kuziingiza nchini ni tatizo.

Sasa sijui kwa kiasi gani sheria yetu hii itaweza kuyafanya haya makampuni pamoja na wafanyabishara binafsi ambao mmoja mmoja wameanzisha makampuni ya biashara kuweza kudhibiti biashara zao hizi ili wasituingizie biashara zenye madhara, kama vile biashara za maziwa ya unga zilizokuwa zimeingizwa miaka ya nyuma.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kabisa ni kwamba sheria hii lazima iweke kwa kushirikiana na hii *ZBS* iweze kutuokoa, mazingira. Kuna baadhi ya kampuni hivi sasa, baadhi ya wafanyabiashara hivi sasa wanatuharibia mazingira kutokana na biashara wanazoleta.

Kwa mfano hivi sasa Mhe. Mwenyekiti, mbali ya kukumbana na lile tatizo la kunguru weusi ambao kwa kiasi kikubwa Mhe. Fatma Fereji Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, lakini sasa ajitayarishe kupambana na mende. Sasa sijui Mhe.Waziri atakapokuja hivi sasa kuna biashara chakavu yanayokuja yale mafriza kutoka Uingereza wana mende wengi wale wadogo wadogo. Sasa sijui ni kiasi gani sheria hii itadhibiti biashara za kampuni ile. Kwa kweli hivi sasa tatizo la mende limekuwa kubwa. Kuna baadhi ya biashara za *electronics* yana zebaki ambayo ni tatizo kwa afya zetu. Sasa nadhani sheria hii itakaposainiwa na Rais basi inaweza ikaleta ukombozi wa hilo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi niende katika suala zima la masharti haya ya biashara. Katika kifungu cha 255 kwenye ukurasa wa 135, "Lengo la biashara ni kuongeza nguvu kwa kampuni na kuongeza uchumi wa nchi".

Mhe. Mwenyekiti, katika hili sijui sheria hii itadhibiti kiasi hizi *briefcase campanies* kwa sababu kuna kampuni za kwenye *briefcase*, kwa mfano mimi miaka nilianzisha kampuni yangu ya mkobani ya ujenzi na nilikuwa nikipata kazi. Lakini nikichelewa kulipwa, ina maana na wale wafanyakazi wangu hawana mishahara. Sasa huo ni usumbufu.

Sasa ni kiasi gani sheria hii itatudhibiti sisi waanzishaji wa makampuni ambayo ni ya maskini ya Mungu. Mimi nilikuwa nafikiri kwamba sheria hii sio tu itudhibiti lakini iangalie sisi wenye muelekeo na moyo wa kuanzisha hizi kampuni hizi. Uzoefu wetu unaonesha katika kuanzisha kampuni hizi kwenye fani zetu basi sheria hii ingeweka kwamba wanaoanzisha kampuni wazalendo basi waweze kupata kiasi fulani cha mkopo wa serikalini ili kusudi kuweza kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Hii itasaidia sana Mhe. Mwenyekiti, kuliko kuendelea kung'ang'ania makampuni ya Wachina tu, wakati sisi mambo ya ujenzi tunayaweza lakini tatizo letu ni umaskini. Sasa mimi nadhani katika kuanzisha kampuni sisi wazalendo tuonekane kwamba iweze katika sheria hii itie kwamba wafanyabiashara wazalendo na wao waweze kupata mikopo nafuu katika kuanzisha makampuni hayo.

Mhe. Mwenyekiti, jengine katika hili lazima serikali iwe makini kwenye kuanzisha kampuni, kwa sababu safu ya watendaji katika kampuni hizi lazima iwekwe wazi. Mimi nilianzisha kampuni ya ujenzi lakini mimi mwenyewe ni mwalimu, sina *engineer* hata mmoja katika kampuni yangu ile iliyokuwa lakini kazi ilikuwa napata.

Sasa ni hatari. Kwa hivyo nilikuwa naomba kwamba katika hili tuwe na *feasibility study* ya hizo kampuni, sio kwamba watu wapewe leseni ya kuanzisha makampuni katika fani hizi hasa zinazohitaji wataalamu, waangaliwe ile *technical team* yake ikoje huyo muanzishaji wa kampuni, sio apewe tu kama mimi huku ni mwalimu nakuja kupewa jengo kama hili, siku mbili tatu ninaanza kukudondosheeni madongo. Sasa hili ni lazima Mhe. Mwenyekiti, tuwe makini.

Mimi sina wasi wasi na kampuni hizi za ususi na *saloon* kwa sababu wale Wamasai wengi wanaweza kufanya mambo ya *saloon*, lakini tatizo ni hizi kampuni zinazohitaji wataalamu wa hali ya juu. Mambo ya kusuka Wamasai wapo lakini sheria lazima iwe makini kwenye hili.

Nadhani Mhe. Mwenyekiti, nimalizie tu kwamba mtu mmoja mmoja sasa anakuwa kampuni. Hivi juzi juzi hapa petu pale Chake Chake kuna bwana mmoja sitaki nimtaje alikuwa akipita akisema anataka kuanzisha kampuni ya kupambana na malaria, lakini lazima upate kazi katika kampuni hiyo utoe shilingi elfu hamsini. Wapemba kule wa kuanzia Mkoani mpaka Konde wakawa wanakusanyishwa shilingi elfu hamsini Mhe. Mwenyekiti, ili kwamba atakapoanzisha kampuni hiyo ya ugawaji vyandarua, kutia dawa majumba wapate ajira.

Matokeo yake Mhe. Mwenyekiti, kampuni ile haikuanzishwa wala fedha za wananchi wale hazikurudi tena na yule bwana aliyekuwa akizikusanya anaonekana anadunda tu huku mitaani. Sasa mimi nilikuwa ninafikiria Mhe. Mwenyekiti, katika hili vile vile hii ya mtu mmoja moja hii ni tatizo, ingawa wapo. Kwa mfano ipo ya SSB & Co lakini na watu wa kawaida nao ni lazima muwaangalie, wasije kufanya mambo kama alivyofanya huyo jamaa, naogopa kuzungumza sana nikaja kumtaja lakini kawadhulumu sana hao vijana, lakini kawadhulumu sana jamaa, kawanyang'anya pesa zao, hakuna ajira iliyopatikana almuradi mashaka tu.

Baada ya maneno hayo machache Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa na unyenyekevu wa hali ya juu, mimi ninaamini mswada huu utatusaidia sana katika suala zima la kuboresha mambo yetu ya makampuni haya na ninaunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia mswada ulio mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu wingi wa rehma aliyetujaalia kuja hapa leo kufanya shughuli zetu hizi kuwa wazima wa afya. Lakini la pili nikushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii.

Mhe. Mwenyekiti, napenda vile vile kuipongeza hususan kumpongeza Waziri pamoja na watendaji wake. Kwa kweli kwa kutuletea mswada huu ambao kwa muda huu unahitajika hasa katika shughuli zetu za kukuza uchumi wa nchi yetu pamoja na vile vile kuwapongeza wana kamati wa Baraza ya Kamati ya Katiba na Sheria, vile vile kwa kuukalia vizuri sana mswada huu na kuweza kufanikisha marekebisho mbali mbali katika mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitokuwa na mengi ya kusema kwa sababu wenzangu waliotangulia tayari wameshachangia vizuri na mimi naungana mkono nao kabisa katika yale ambayo wameyachangia. Nitaanza katika ukurasa wa 157.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa huo kuna suala zima katika kifungu cha 239 (c) kidogo Mhe. Mwenyekiti, hapa nilikuwa kimenitia wasi wasi hiki kifungu cha (c) kinachozungumzia masuala mazima ya kampuni zilizoandikishwa nje ya Zanzibar.
Kifungu cha (c) kinasema kwamba "Majina na anuwani za baadhi ya watu mmoja au zaidi ya wakaazi wa Zanzibar walioidhinishwa kukubali kwa niaba ya kampuni kuhudumia

mwenendo na taarifa yoyote iliyotakiwa kutolewa kuhusu kampuni".

Mhe. Mwenyekiti, khofu yangu kubwa hasa ni kwamba wakati kampuni ambayo itakuwa imesajiliwa nje, ina maana ni lazima iwe na mawakala wake hapa Zanzibar. Lakini hili suala la kusema kwamba wakaazi wa Zanzibar, kidogo imenitia khofu.
Kwa sababu nafikiria mustakabali mzima wa Wazanzibari wenyewe ambao wanaweza kushirikishwa moja kwa moja katika kampuni hii. Tukisema mkaazi tunafahamu nini maana ya mkaazi, ni yule ambaye anaweza kuwa ni mtu wa sehemu nyengine lakini akawa na ukaazi wa Zanzibar.

Sasa mimi nilikuwa nataka nijue Mhe. Waziri hapa tunakusudia nini, tunaposema kwamba mkaazi wa Zanzibar. Jee, huyu mwenye Zanzibar hasa atashirikishwa vipi? Lakini jengine vile vile ambalo nimeliona katika ukurasa huu huu wa 157, katika kifungu kidogo nambari 2. Hii hapa ni lugha ambayo imetumika. Mhe. Waziri ninavyofahamu mimi *paragraph* ina tafsiri yake, *paragraph* ni kwa Kiingereza, *paragraph* ni aya.

Sasa tujitahidi sana katika lugha hizi tusitohoe kutoka kwenye Kiingereza tukakipeleka kwenye Kiswahili tutakuwa tunafanya makosa, kwa sababu neno lile limo katika Kiswahili na nafikiri ingekuwa vizuri zaidi ikawekwa kama aya badala ya kuwekwa *paragraph*. Sijaona katika maeneo mengine lakini hiyo nilikuwa naomba sana tutahadhari wakati tunapotafsiri miswada hii kuhakikisha kwamba Kiswahili ndicho kinachotumika katika miswada yetu; ya Kiingereza itabakia kuwa ni ya Kiingereza lakini ya Kiswahili tuhakikishe kwamba inachukua yale maneno ambayo mtu yeyote anaweza kufahamu maana ya neno lile.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka kwenda moja katika ukurasa wa 165. Katika ukurasa huo nalisema hili Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu tumekuwa tunalizungumza sana katika miswada yetu mingi, tunalisema hili neno "Waziri anaweza".

Neno hili Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe mara nyingi tumekuwa tunalikataa, "Waziri anaweza" na sijui kwa nini linakuwa linajirejea. Kuna baadhi ya maeneo ni kweli kwa sababu tunampa *options* Waziri aidha atumie ile haki yake au anaweza asitumie. Lakini kuna baadhi ya maeneo ni kitu cha lazima Waziri anatakiwa kufanya vile, sio kwamba Waziri anaweza.

Tunaposema kwamba Waziri anaweza, maana yake tumemwambia Waziri hata siku moja hatuwezi kumuuliza hapa kwa nini hukufanya. Lakini kuwe na uwezekano kwamba Waziri anatakiwa afanye jambo fulani. Sasa ukitazama kifungu kidogo cha 2 "Waziri anaweza kuteua wasajili wasaidizi kama yeye anadhani ni lazima pale ambapo watahitajika" ndio maana hiyo. Lakini kwa mtizamo wangu mimi Waziri atatakiwa kupata wasaidizi. Sasa hapa mimi nina wasi wasi mkubwa lakini katika kifungu hicho hicho (4), "Waziri anaweza kuagiza muhuri utayarishwe kwa ajili ya uthibitishaji wa nyaraka zinazohitajika kwa ajili au kuhusiana na usajili.

Sasa mimi nafikiria suala la muhuri ni suala la lazima halitaki kwamba Waziri anaweza. Lakini vile vile kuna suala la Waziri anaweza kushauriana, na hilo nafikiri vile vile Waziri anaweza pia kushauriana na Mrajis anaweza kutunga Kanuni, kuweka ada zinazopaswa kulipwa.

Sasa mimi Mhe. Waziri nilikuwa naomba sana hasa labda sisi Waheshimiwa Wajumbe huku nyuma hatujafahamu maana ya *anaweza*. Hebu tupeni hii tafsiri ya *anaweza* maana yake. Ina tofauti sana na kumtaka mtu afanye kazi yake ambayo anatakiwa kufanya na kumwambia afanye kama anataka kama hataki basi aache.

Mhe. Mwenyekiti, umuhimu wa mswada huu ni mkubwa sana. Katika maendeleo ya binadamu tunapitia mabadiliko mbali

mbali, na mabadiliko yale ni kutoka hatua moja na kwenda hatua nyengine. Nikiwa na maana hatua ya maendeleo. Sote tunapitia hatua ambayo tunaita *evolution*, ni muhimu sana. Na hili litafanyika tu pale ambapo sisi tutakuwa tayari kulifanya na jambo lolote kuwa tayari kulifanya, maana yake ni kuliwekea mazingira mazuri.

Katika kuweka mazingira mazuri, kitu muhimu sana watendaji hawa ambao tutawapa jukumu hili waweke mazingira ya kuweza kufanya kazi zao vizuri. Bila ya hilo Mhe. Mwenyekiti, tutakuwa sheria zetu nyingi tunazichukua na kuziweka katika makabati lakini hazifanyi kazi na matokeo yake matunda hayaonekani.

Sasa hivi Tanzania tunazungumza Mhe. Rais Kikwete amesema tunataka *big result*, matokeo makubwa mazuri. Lakini kama hatujatengeneza msingi si rahisi kuyapata. Mhe. Mwenyekiti, mimi ningemuomba sana Mhe. Waziri kuna baadhi ya sheria hizi pamoja na nyengine zote zinatakiwa kufanyiwa ukarabati hasa katika lugha ambayo inatumika ili wananchi waweze kuielewa vizuri. Tunataka lugha ambayo itakuwa ni rafiki kwa wananchi, lugha ambayo mtu yeyote akisoma anafahamu hasa katika kuwapelekea wananchi. Ningemuomba sana Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri hili alitilie maanani.

Lakini la pili sheria hizi zinaweza kwenda katika daraja zikafundishwa na zikaanza kutolewa kuanzia skuli ya msingi mpaka kufikia Vyuo Vikuu. Mheshimiwa mwenzangu amesema pale kwamba ipo haja wanafunzi wa Vyuo Vikuu wakapewa taaluma hii. Nakubaliana na yeye asilimia mia kwa mia.
Lakini kuanza chini ni muhimu sana. Tunaweza tukadondoa vitu vidogo vidogo kwa kutengeneza lugha nyepesi kabisa ili watoto wetu wanaokuwa, wanaweza kuwa na uelewa mzuri wa fursa ziliomo ndani ya nchi yao. Makosa makubwa tunayafanya, elimu kubwa inatolewa katika ngazi ya juu na hili ni tatizo. Kwa hivyo tunahitaji Mhe. Mwenyekiti, katika masuala yote ya sheria shirikiana sana na Wizara ya Elimu kuhakikisha kwamba msingi

wa sheria hizi zote ambazo zinakuja zinaanzia kwa watoto wetu wadogo, akifika elimu ya juu anazifahamu fursa zote ziliomo ndani ya nchi yake na kuweza kuzitumia vilivyo.

Tatizo kubwa linajitokeza kwamba mara nyingi sana vijana wetu sasa hivi wapo tunasema hakuna kazi, hakuna ajira. Lakini ukweli hawajui fursa zilizopo ambazo zimetengwa kwa ajili yao. Na hii ni kukosekana kwa kutojua sheria. Kwa hivyo mimi pamoja na kuipongeza wizara yako lakini naiomba sana wizara yako Mhe. Waziri ishirikiane na wizara zinazohusika na kuhakikisha kwamba inamtengenezea Mzanzibari, kijana, mtoto na wengine wote mazingira mazuri ya kuweza kupata fursa ambazo zimeletwa kwa ajili ya Wazanzibari.

Lakini licha ya hayo Mhe. Mwenyekiti, ningependa tu katika suala ambalo nimeshalizungumzia zaidi ni kuhusu elimu kwa jamii, ningeomba sana na najua kuna kazi ambazo zinafanywa, lakini vile vile elimu itolewe kwa viongozi wetu, tunasema *local authority*, wale na wao wanabeba jukumu kubwa sana la kuwasaidia wananchi katika kujua haki zao pamoja na fursa zilizopo.

Tumeona wananchi wetu wameingizwa katika mikataba ambayo kwa kweli mikataba ile imewapeleka wananchi pabaya na leo hawana pa kwenda. Lakini kwa sababu kwamba viongozi wapo katika maeneo yao wameshindwa kuwasaidia wale kuanzia mwanzo, hili limekuwa ni tatizo.

Moja ya tatizo ni kwamba kwanza wengi wao sheria hawazijui, utaratibu hawaujui, lakini la pili rushwa imefanya kazi kubwa katika kuwaingiza pabaya wananchi. Kwa hivyo mimi ningeomba sana Mhe. Mwenyekiti, serikali zetu za mitaa pamoja na sheria hizi tunazitayarisha ziwe na uelewa mkubwa ambao utasaidia katika kutekeleza sheria hizi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitokuwa na zaidi ya kusema, hayo ni yangu niliyokuwa nayo. Naipongeza tena wizara na nawatakia kila la kheri katika utekelezaji. Naomba Mhe. Mwenyekiti, watendaji kwamba watekeleze kwamba waweke mazingira mazuri lakini nataka niwaambie tu wenzetu hivi karibuni nchini Kenya kama niliona na kufahamu watendaji wakuu wa serikali wameanza kufungishwa mikataba ya utendaji. Hii itasaidia sana katika utendaji.

Wanafungwa mikataba kwa sababu atakapokuwa atashindwa kufika pale ambapo ametakiwa kufika anaondolewa. Tena anaondolewa na yule mtu anakuwa hafai kabisa katika kazi zile. Nafikiria Mhe. Waziri utakubaliana na mimi tunakaribia kufika huko. Kuna watendaji hawafai, wapo tunawalea ni tatizo kubwa, na kumlea mtu mmoja, ukamnusuru mtu mmoja ukaangamiza kundi la watu wengi, kwa kweli ni uhaini mkubwa. Kwa kweli sivyo na wenzetu Kenya wameshaanza na sisi tuwe tayari kufanya hivyo ili tufanikiwe, laa hatukufanya hivyo tunaharibu maendeleo yetu pamoja na maendeleo ya kizazi kijacho.

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa lakini ninakukumbusha tu Waheshimiwa Wajumbe walikuwa na ombi lao, kwa hivyo kabla ya kufunga hapa unatakiwa utoe fat-wa ya lile ambalo limeombwa.Ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mwenyekiti mwenza kwa kunikumbushia ombi la Wajumbe tokea asubuhi, lakini pia nikushukuru kwa namna ulivyomalizia na zaidi namna ulivyojali muda, na pia nichukue fursa hii kuwashukuru sana Wajumbe kwa namna tulivyoshirikiana hadi kuweza kufikia hapa ambapo katika orodha yangu sina mchangiaji mwengine wa ziada.

Sasa nafasi iliyobakia ilikuwa ni nafasi ya Mhe. Waziri tu peke yake ili aweze kutoa majumuisho na baadae tupitishe vifungu. Lakini kwa mujibu wa muda ambao tulionao kwa sasa, hilo litakuwa haliwezekani kwa sasa na vile vile tukizingatia Kanuni

kifungu cha 85(1) kinampa nafasi Mhe. Waziri ya kupewa muda wa masaa sita ili aweze kujiweka tayari kwa ajili ya kutoa majibu ya hoja ambazo zimewasilishwa na Wajumbe.

Sasa bila ya kupoteza muda niseme kwamba tutoe muda huo na niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wenzangu tuakhirishe Baraza hili hadi siku ya Alhamis tarehe 17 Oktoba, 2013 saa 3: 00 za asubuhi na kumkaribisha Mhe. Waziri baadae aje kutoa majumuisho ya mswada huu.

Baada ya maelezo hayo nachukua fursa hii kuakhirisha Baraza hili hadi siku ya Alhamis.

(Saa 6:55 mchana Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 17/10/2013 saa 3:00 asubuhi)